# Nipashe Jumapili

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • No. 0581702

Jumapili Juni 9, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

& FOLLOW US




**Makonda** apiga 'stop' ukaguzi magari watalii

UKURASA 2



**Elimu** mikopo kausha damu yashika kasi

UKURASA 5



**ACT** yalia ugumu wa maisha kwa wahitimu

UKURASA 8



WEKA SAFI MIDOMO

UK. 14

# Utata mzito nyumba mstaafu kubomolewa

• **Ni** kwa amri ya mahakama, adai ana hati, amwangukia Waziri Silaa... *uk 2*




Mwalimu mstaafu mjane, Amina Mghenyi, akiwa nje ya nyumba yake ambayo mahakama imeamuru ibomolewe. **PICHA THOBIAS MWANAKATWE**

# Ziara ya Nchimbi yasomba 400 kutoka upinzani

UKURASA 3



**Na Romana Mallya,**
TANGA

ZAIDI ya wanachama 400 wakiwamo waliokuwa wagombea ubunge, madiwani na wenyeviti wa wilaya kutoka vyama vya upinzani, kikiwamo Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) wametangaza kujiengua na kujiunga Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Wanachama hao wametangaza kuhamia CCM ...

## YALIYOMO

UKURASA WA 7

### WALIMU WAPEWA MBINU KUHUSU UFUNDISHAJI



NAIBU Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia Elimu, Dk. Charles Msonde, amesisitiza walimu wa shule za msingi na sekondari nchini kuzingatia uwezo wa wanafunzi wanapofundisha...

UKURASA WA 7

### SERIKALI YASHAURI WATOTO WAFUNDWE UWEKAJI AKIBA

# HESLB yaanika utaratibu upangaji mikopo wanafunzi

UKURASA 2

**MICHEZO** YANGA SC KUTIKISA NCHI LEO UK.24

**MAONI,** UK.6

## HESLB yaanika utaratibu upangaji mikopo

**Na Mwandishi Wetu**

Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) imetoa ufafanuzi kuhusu utaratibu unaotumika katika uchambuzi na upangaji wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu na kusema upangaji huo huzingatia uhitaji wa mwombaji na kuwa si waombaji wote hupata asilimia 100.

Ufafanuzi wa HESLB unatokana na taarifa iliyochapishwa na gazeti hili juzi kuwa kuna uwezekano baadhi ya wanafunzi hawatapata mikopo kwa asilimia 100 kutokana na bajeti iliyotengwa ya Sh. Bilioni 787 kwa wanafunzi 250,000 katika mwaka wa masomo 2024/25.

"Upangaji mikopo ya elimu inayotolewa na HESLB huzingatia uhitaji wa mwombaji mkopo ambao hupimwa kwa taarifa anazojaza wakati wa maombi, hivyo si kila mwombaji ana uhitaji wa asilimia 100," alisema Meneja Mawasiliano wa HESLB, Venerranda Malima.

"Kwa mfano, miongozo yetu inaeleza kipaumbele hutolewa kwa waombaji wenye ulemavu, yatima na wale ambao wanatoka katika kaya zinazohudumiwa na TASAF, waombaji kutoka katika makundi haya huwezi kuwalinganisha na waombaji wa kawaida, waombaji hutofautiana uwezo na uhitaji," aliongeza Malima.

Juzi, Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Dk. Bill Kiwia, alitangaza kufunguliwa kwa dirisha la kuomba mikopo kwa njia ya mtandao kwa siku 90 kuanzia Juni Mosi hadi Agosti 31, mwaka huu.

Dk. Kiwia alisema mwombaji mkopo anapaswa kuingia katika tovuti rasmi ya HESLB (www.heslb.go.tz) na kubofya sehemu ya kuomba mkopo, atajisajili huko kwa kutumia namba yake ya Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne na kufuata maelekezo.

Nipashe katika toleo lake la juzi ilisema katika wa masomo wa 2024/25, dirisha kwa ajili ya mikopo kwa wanafunzi wanaotarajiwa kujiunga na masomo ya vyuo vikuu limefunguliwa kwa wanafunzi 250,000 wanaotarajia kunufaika na fursda hiyo.

Hilo ni ongezeko la wanafunzi 25,944 kulinganishwa na wanufaika 224,056 wa mikopo hiyo kwa mwaka wa masomo 2023/24. Pamoja na kuonyesha kiasi cha fedha na idadi ya wanafunzi, Nipashe ilifanya uchambuzi na kubainisha kuwa ata hivyo, kiasi kilichotengwa kwa ajili ya utoaji mikopo hiyo kinazua utata na kutoa ishara kwamba wanufaika wengi hawatopewa mkopo kwa asilimia 100.

Kwa mujibu wa uchambuzi huo, katika lugha ya hisabati, Sh. bilioni 787 zilizotengwa na serikali kwa ajili ya mikopo kwa wanufaika 250,000 zina maana kutatolewa mkopo wa wastani wa Sh. milioni 3.148 kwa kila mnufaika.

Uchambuizi huo ulionyesha kuwa ni ishara kwamba wanafunzi wengi hawatapewa mkopo kwa asilimia 100 kwa kuwa fedha kwa ajili ya kujikimu ni Sh. milioni 2.4 kwa mwaka (Sh. 10,000 kwa siku).

Ukitoa Sh. milioni 2.4 katika fungu la wastani wa Sh. milioni 3.148 kwa kila mnufaika, kitabaki kiasi cha Sh. 748,000 ambacho ndicho mwanachuo atalazimika kukitumia kama kianzio kulipa ada ya chuo, mafunzo kwa vitendo (PT), utafiti, vitabu na vifaa vingine vya darasani.



Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Camillus Wambura (katikati), akizungumza wakati akikagua mradi wa ujenzi unaoendelea wa jengo la Kamanda wa Mkoa wa Kipolisi Rufiji, mkoani Pwani jana. **PICHA: JESHI LA POLISI**

# Utata watanda nyumba ya mstaafu kubomolewa

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

UTATA umeibuka baada ya mahakama kutoa amri ya kuvunjwa kwa nyumba ya mwalimu mstaafu na mjane mkoani hapa, Amina Mghenyi, ambayo ilitolewa mwaka 2012 na kutakiwa kutekelezwa sasa.

Hali hiyo ya utata inatokana na mwalimu huyo mstaafu kuwa na hati ya umiliki wa eneo na kulipa kodi ya ardhi kisheria na kuambiwa kuwa aliuziwa eneo ambalo lilikuwa na mgogoro.

Amri hiyo ya mahakama inatokana na hukumu ya kesi iliyotolewa na mahakama ambayo anasema hajawahi kuitwa mahakamani hata siku moja.

Kutokana na hali hiyo, mstaafu aliyeitumikia serikali kwa miaka 39, amemwomba Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa, kuingilia kati baada ya nyumba yake kutaka kubomolewa kwa agizo la mahakama.

Akizungumza na waandishi wa habari jana katika nyumba hiyo iliyoko eneo la Mahambe, Manispaa ya Singida, Mghenyi alisema nyumba yake hiyo imewekewa alama ya X ambayo inatakiwa kubomolewa Juni 16, mwaka huu.

Alisema kiwanja alichojenga nyumba yake alikinunua Juni 16, 2018 kwa Sh. milioni 17 kwa John Gwau ambaye ni marehemu na kupewa hati namba 573 na tangu alipokinunua na kujenga nyumba, amekuwa akikilipia halmashauri kama taratibu na sheria zinavyoelekeza.

Mghenyi alisema katika hali ya kushangaza, Mei 31, mwaka huu nyumba yake iliwekewa alama ya X na dalali wa mahakama kutoka kampuni ya Taomtra Limited na kutakiwa kuibomoa mwenyewe Juni 15, 2024 na asipofanya hivyo, ifikapo tarehe hiyo litapelekwa tingatinga na kuibomoa.

Alisema kinachomshangaza ni kwamba kesi ambayo ilipelekwa mahakamani na mlalamikaji, Suzana Mahami, kuhusu kiwanja cha nyumba hiyo, hajawahi kuitwa mahakamani na wala hakuwa mshitakiwa katika kesi hiyo.

Mahami, ambaye ni mlalamikaji katika kesi hiyo, alisema ni kweli mwalimu huyo hakuhusika katika kesi aliyoipeleka baraza la ardhi bali alimshtaki aliyeuza kiwanja hicho palipojengwa nyumba ya mwalimu huyo kwa kuwa aliuziwa eneo hilo kinyume cha sheria na utaratibu.

Alisema kimsingi mwalimu huyo, kesi hiyo imemgusa kwa sababu amejenga nyumba yake katika kiwanja ambacho kilikuwa na mgogoro bila yeye kujua. "Mimi kimsingi sina tatizo na mwalimu huyo.

Ninachotaka kama atataka nilipwe gharama zangu za kesi na kupewa kiwanja kingine halafu mimi nitamwachia eneo hilo alipojenga nyumba yake," alisema Mahami.

Naye Sixmund Gwau ambaye ni mtoto wa John Gwau aliyeuza kiwanja hicho kwa mwalimu huyo mstaafu, alisema baba yake alipouza eneo hilo, hakukuwa na mgogoro wowote na kusisitiza kuwa mwalimu huyo aliuziwa kihalali kwa kufuata taratibu zote.

Naye Balozi wa Mtaa wa Mahembe, Asia Hamis, alisema serikali iangalie namna ya kumsaidia mwalimu huyo mstaafu na mjane kwa kuwa kama nyumba yake itabomolewa, familia yake ataipeleka wapi, amezeeka na hana nguvu za kufanya kazi kupata pesa za kujenga nyumba nyingine.

Diwani wa Kindai, Imari amis, alisema tangu 2015 alipoingia kwenye udiwani, hajawahi kusikia eneo hilo lina mgogoro na kinachoshangaza hukumu ya kesi hiyo ilitolewa tangu 2012 halafu utekelezaji wake unafanyika mwaka huu kitu ambacho kinatia shaka.

"Naiomba serikali na mahakama imsaidie mjane huyu kuokoa maisha yake kwani nyumba yake ikibomolewa na hali aliyokuwa nayo ni wazi kuwa kutasababisha maisha yake kuwa magumu sana," alisema.

Mwenyekiti wa Baraza la rdhi Singida, Bahati Colex, alisema hukumu ya kesi hiyo ilitolewa katika Mahakama ya Kuu Dodoma na wao walipewa amri na kumtafuta dalali wa mahakama kwa ajili ya kutekeleza kuibomoa nyumba hiyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taomtra Limited, Salim Adam, alisema wakiwa madalali wa mahakama walipewa kazi hiyo ya kutaka kubomoa nyumba hiyo na Baraza la Ardhi.

# Makonda apiga 'stop' ukaguzi magari watalii

**Na Beatrice Shayo**, ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda, ameagiza polisi kuacha kusimamisha magari ya watalii yanayoingia katika jiji la Arusha kuanzia Julai Mosi, mwaka huu.

Amesema magari hayo yanapoingia Arusha yanakuwa tayari yameshakaguliwa katika mipaka na viwanja vya ndege.

Makonda alitoa agizo hilo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari katika maonyesho ya Karibu Kili Fair (KKF) yanayofanyika katika viwanja vya Magereza Kisongo, yakijumuisha zaidi ya kampuni 700 za kimataifa kutoka zaidi ya nchi 50.

"Tumekubaliana kuanzia Julai Mosi, mwaka huu, hakuna polisi kusimamisha magari yaliyobeba watalii kutoka airport (uwanja wa ndege) au Namanga kuingia katikati ya jiji la Arusha," alisema.

Makonda alisema wanafanya hivyo kwa sababu watalii hao wanakuwa tayari wameshakaguliwa kwenye viwanja vya ndege au mipakani, hivyo hakuna sababu ya kuwekewa vikwazo kwa kuwa wengine wanawahi ndege au ratiba zao. "Hawa watalii wamekuja kutupatia fedha kutokana na kazi kubwa iliyofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan kwa ukarimu aliouonyesha kwao lazima watu wa mkoa wa Arusha waonyeshwe kwa ukarimu," alisema Makonda.

Alisema vyombo vyote vinavyohusika na ukaguzi wa wageni, vifanye kwenye vituo vya mipaka na viwanja vya ndege.

Aidha, Makonda alitoa miezi miwili kwa teksi zinazotumika kubeba wageni na watalii wa mkoa wa Arusha kuwa na rangi maalumu za kufanana ili kutoa urahisi kwa watalii kulifahamu gari hilo na usalama kwa wageni na watalii wanapoamua kutumia aina hiyo ya usafiri wanapokuwa jijini Arusha.

Makonda alisema wataendelea kuunga mkono jitihada za Rais Samia za kuvitangaza vivutio vya utalii vilivyopo nchini Tanzania na kutaka kila mmoja kwenye eneo lake la kazi kuonyesha ukarimu kwa vitendo kila wanapokuwa wanahudumia wageni.

# Ziara ya Nchimbi yazoa 400 upinzani

**Na Romana Mallya,** TANGA

ZAIDI ya wanachama 400 wakiwamo waliokuwa wagombea ubunge, madiwani na wenyeviti wa wilaya kutoka vyama vya upinzani, kikiwamo Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) wametangaza kujiengua na kujiunga Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Wanachama hao wametangaza kuhamia CCM wakati wa ziara ya Katibu Mkuu CCM, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, iliyohusisha mikoa mitano ya Singida, Manyara, Arusha, Kilimanjaro na Tanga iliyomalizika jana.

Katika Jimbo la Korogwe Mjini, aliyekuwa mgombea ubunge kwa tiketi ya Chama Cha Wananchi (CUF) mwaka 2020, Amina Magogo, wenyeviti na madiwani tisa wametangaza kuhamia CCM pamoja na aliyekuwa mgombea ubunge kupitia Chama cha ADA TADEA Singida.

Korogwe pekee, wanachama waliotangaza kujiunga chama tawala ni 225, akiwamo Mwenyekiti wa CUF Wilaya ya Korogwe, Nurdin Abubakar.

Akizungumza juzi katika mkutano wa hadhara siku moja kabla ya kuhitimisha ziara yake katika mikoa hiyo, Balozi Nchimbi alisema kazi za Rais Samia Suluhu Hassan ndizo zinazovutia wengi kurejea CCM.

Balozi Nchimbi alisema ziara aliyofanya katika mikoa hiyo imewezesha kuvuna wanachama hao kutoka upinzani kujiunga na chama tawala.

"Tunawashukuru ndugu zetu hawa ambao wameamua kwa hiari yao kujiunga na Chama Cha Mapinduzi na kwa kweli wameingia kwa kishindo maana si kwa wingi huu," alisema.

Awali, akizungumza kwa niaba ya wenzake, Magogo alisema amechukua uamuzi huo baada ya kuona juhudi zinazofanywa na Rais Samia, hivyo kumridhisha na kumwahidi Katibu Mkuu CCM kuendelea kuvuna wanachama wengine.

Akihutubia wananchi, Balozi Nchimbi alisema katika miaka mitatu ya Rais Samia, yamefanyika mambo makubwa ambayo hayajawahi kutokea.

Alisisitiza kwamba ziara hiyo wameifanya kwa ajili ya kuangalia uhai wa chama, kuangalia utekelezaji wa ilani na kusikiliza kero mbalimbali na mpaka sasa tangu wameanza huo ni mkoa wa 10.

Aidha, alisema jambo linalotia faraja ni taarifa za utekelezaji wa ilani, mabadiliko waliyoona katika miradi ya elimu, afya, barabara na maji ambayo yamefanyika katika kiwango ambacho hakijawahi kutokea tangu historia ya nchi.

"Kwa miaka mitatu mambo yaliyofanyika hayajatokea na hii ni heshima kubwa kwa wanawake, Rais Samia amewapa heshima kubwa wanawake si tu wanawake wa Tanzania bali wanawake wa dunia nzima, hofu na mashaka ya watu siku zote kwamba wanawake hawawezi imekwisha.

"Tumejiridhisha pasi shaka kwamba, mwanamke ukimpa nafasi anatumia uwezo anaotumia kama kwenye familia anakuwa mama wa taifa, ndio maana Rais wetu amekuwa akisimamia ukusanyaji wa mapato ya ndani ambao umeongezeka mara dufu tangu amekuwa Rais," alisema.

Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo CCM Taifa, CPA Amos Makalla, alisema upinzani hawaaminiki wamekuwa watu wa kuzua mambo na uchochezi na hivyo kuwatofautisha kati ya CCM na vyama vya upinzani.

"Ukiwauliza tunakwenda katika uchaguzi utawaambia nini wananchi ili wawaamini wanasema wanayo mambo matatu, ajenda yao ya kwanza watakwambia, 'katika mambo tuliyofanya vizuri nchi nzima tumekuwa na mpango kazi wa kufanyika maandamano' maandamano yanaleta maendeleo? Yametatua kero? " alihoji wananchi.

Makalla alisema itapasuka wakati wowote ndiyo maana wanazua mambo ili kuficha mgogoro uliopo.

"Mimi za ndani nilizonazo wakati wowote tutaanza kupokea viongozi wakubwa wa CHADEMA kwenda vyama vingine na wengine kuja Chama Cha Mapinduzi," alisema.



Katibu Mkuu CCM, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi akiwa katika moja ya ziara zake.


## Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya epaper.ippmedia.com utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza "subscribe"
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa kadi ya benki malipo kwa mtandao wa simu unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa namba ya simu unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. Kwa benki unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

6. Unafungua website yako ya www.ippmedia.com upande wa kulia utaona "E-Paper" utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian



Mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa wa Mara, Moses Kaegele, akizungumza katika uzinduzi wa mashindano ya uchomaji nyama 'Nyama Choma Festival', huko Kiabakari, wilayani Butiama juzi, ikiwa ni sehemu ya kutambulisha shughuli za uchumi za mkoa huo ikiwamo ufugaji ng'ombe. **PICHA: SABATO KASIKA**

# CCM yageukia ufufuaji viwanda Tanga

**Na Romana Mallya,** TANGA

WAKATI serikali ikianika mikakati yake ya kuvifufua viwanda vilivyokufa mkoani Tanga kwa kuwaita waliovinunua ili kuvifufua, Chama Cha Mapinduzi (CCM) kimesema uwekezaji huo utajenga uchumi imara na nchi kwa kuongeza upatikanaji wa fedha za kigeni.

Akizindua kiwanda cha kuzalisha nyaya za umeme cha Tanga Cable mkoani hapa kwa ajili ya kuunganisha umeme vijijini ukanda wa Kaskazini-Mashariki, Katibu Mkuu wa CCM, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, alitaka bidhaa za ndani ziungwe mkono.

Balozi Nchimbi alitoa wito kwa taasisi mbalimbali za serikali na sekta binafsi kutumia bidhaa zinazozalishwa nchini kupitia viwanda vilivyopo na vinavyoanzishwa.

Alisema wanahitaji viwanda vya ndani si kwa ajili ya mapambo bali kujenga uchumi.

Balozi Nchimbi alitaka jitihada zinazofanywa na wazawa zisipotee bure hivyo, waungwe mkono kwa bidhaa zao kununuliwa.

Alisema uzinduzi wa kiwanda hicho ni utekelezaji wa Ilani ya CCM na kwamba wanatambua kwamba hakutakuwa na mafanikio ya kweli kama sekta binafsi haitashiriki katika ujenzi wa taifa.

Balozi Nchimbi alisema wanapata faraja kuona wazawa wanachukua hatua na kuanzisha viwanda.

"Tunayo changamoto kubwa ya uagizaji wa bidhaa nyingi nje. Tungependa tufike mahali tujitegemee katika uzalishaji wa bidhaa zetu sisi wenyewe ndani, tuwe na viwanda vya kutosha ambavyo vitasaidia kwanza, kubadilisha urari wa kibiashara.

"Kwamba tuwe na uwezo wa kuuza zaidi ya tunavyonunua ili kujipatia fedha za kigeni za kutosha na kuendesha mambo yetu mbalimbali ya uchumi wa nchi," alisema.

Pia alisema kwa kuwa na viwanda kunawezesha upatikanaji wa ajira za kutosha kwa wananchi na kupunguza gharama za usafirishaji ambazo ni kubwa wanapoagiza bidhaa nje.

"Tunawapa shime watanzania wote wenye nguvu za kuwekeza waige mfano wenu na wa wengine waliofanya jambo kama hili ili kujenga viwanda vidogo na vikubwa," alisema na kubainisha kuwa hali hiyo itasaidia kujenga na kuimarisha uchumi wa nchi.

Aliwahakikishia wawekezaji hao kwamba CCM itaendelea kusimamia sera yake ya kuhakikisha sekta binafsi inafanyiwa mazingira ya uwezeshaji ili maendeleo endelevu kupatikana kwa urahisi, lakini kasi ya kukua kwa uchumi wa nchi iwe kubwa zaidi kuliko hivi sasa.

"Nitoe wito kwa taasisi mbalimbali za serikali na sekta binafsi kuona jitihada zinazofanywa na wafanyabiashara wazawa zisipotee bure kwa kadri inavyowezekana tutumie bidhaa za ndani na hasa tukishajiridhisha ubora wake.

"Chama Cha Mapinduzi kitatumia nafasi hii kusisisitiza mara kwa mara kwamba, tunahitaji viwanda vya ndani si kwa ajili ya mapambo, tunavihitaji ili vishiriki kujenga uchumi wa nchi yetu," alisema.

Mkurugenzi wa Tanga Cable, Murtaza Dossaji, alisema kiwanda hicho ni kwa ajili ya kuzalisha nyaya za umeme kwa ajili ya kupeleka na kuunganisha umeme vijijini.

Alisema ni kiwanda pekee katika kanda ya Kaskazini-Mashariki kinachozalisha nyaya hizo za umeme, kilichoanzishwa na wazawa, wakiwekeza zaidi ya Sh. bilioni moja na kinatarajia kuajiri zaidi ya wafanyakazi 50.

"Lengo la kiwanda ni kuboresha sekta ya umeme Tanzania kwa ujumla, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Kanda ya Kaskazini na makandarasi wa REA (Wakala wa Nishati Vijijini) ambao wamepata kazi katika kanda hii watanufaika kwa kupata nyaya kwa bei nafuu na usafirishaji wake utapungua kwa kuwa zipo ukanda huu.,' alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Balozi Dk. Batilda Burian, alisema Tanga ni mkoa uliokuwa ukisifika kwa viwanda, lakini vingi vimekufa na vilivyobinafsishwa vingi vimenunuliwa na kufanywa magofu.

"Hivi vinavyochipuka na kumea wanataka viendelee kushamiri ili kuwa na uchumi mkubwa. Maelekezo ya chama ni kuhakikisha viwanda vilivyobinafsishwa vinafufuka na tayari tumepanga mkakati wa kuwaita walionunua viwanda hivyo vifufuliwe.

"Pia kushawishi wawekezaji wapya kuja kufungua viwanda kwa sasa tuna karibu viwanda vitatu vya saruji na hivyo, tunategemea tuendelee kuwa navyo vingi katika sekta ya uchumi wa buluu na sekta ya kilimo katika kuongeza thamani , madini ujenzi na umeme ikiwamo hiki cha Tanga Cable," alisema.

# Mageuzi yapaisha sekta ya utalii

**Na Cynthia Mwilolezi**, ARUSHA

WAZIRI wa Malisili na Utalii, Angellah Kairuki, amesema maboresho yaliyofanywa na serikali katika sekta ya utalii yamechangia ongezeko kubwa la watalii wa nje ya nchi na ndani wanaotembelea vivutio vya utalii nchini.

Aidha, amewapongeza wadau binafsi wa sekta ya utalii ambao wanafanya kazi kubwa ya kutangaza vivutio vya utalii nchini, wakiwamo Karibu Kili Fair ambao kila mwaka wanafanya maonyesho ya kimataifa ya utalii yanayowakutanisha watoa huduma na wanunuzi katika sekta hiyo.

Waziri Kairuki alisema hayo jana wakati akifungua maonyesho ya Karibu Kili Fair (KKF) ambayo yameshirikisha zaidi ya wanunuzi 600 wa bidhaa mbalimbali za utalii kutoka nchi 42 duniani na wadau wa utalii 468 kutoka nchi 37.

"Mazingira bora ya biashara kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi yamekuwa na tija kubwa katika sekta ya utalii tumeona idadi ya watalii wa ndani na nje ya nchi wakiongezeka kila siku.Nataka niwahakikishie kwamba serikali itaendelea kushirikiana na wadau wa sekta hii muhimu kwa taifa,"alisema Waziri Kairuki na kuongeza kuwa;

"Sekta ya utalii hapa nchini inachangia pato la taifa kwa asilimia 17.2 huku ikichangia asilimia 25 ya fedha za kigeni lakini mafanikio yote haya yanatokana na ushirikiano mzuri wa serikali na sekta binafsi," alisema.

Waziri Kairuki alisema maonyesho hayo ya kimataifa yana tija kubwa kwa kuwa yanawakutanisha watoa huduma za utalii nchini na wanunuzi wa bidhaa mbalimbali za utalii ikwemo safari na hoteli.

"Ni imani yangu kwamba maonesho haya yatawakutanisha wanunuzi na wauzaji wa bidhaa mbalimbali za utalii na yatatoa fursa ya kufanya biashara mbeleni ambayo yatakua na tija kwa taifa," alisema.

Naye Mkurugenzi wa Karibu Kili Fair, Dominic Shoo, alisema amepokea ushauri uliotolewa na kuahidi kuyafanyia kazi kwa kuwa anatambua mchango wao mkubwa katika kukuza sekta hiyo muhimu.

Shoo alisema maonyesho hayo yanawawezesha kukua na kufikia viwango vya kimataifa, wanaomba wadau wa utalii kuendelea kushiriki ili kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan, katika juhudi za kitangaza vivutio vya utalii, katika kufikia masoko ya utalii ulimwenguni.

Mkurugenzi huyo aliomba mawakala wa utalii nchini kuendelea kuunga mkono kwa kushiriki maonyesho hayo ili kuongeza idadi6 ya watalii iweze kufikia milioni tano ifikapo mwaka 2025.

"Lakini naomba Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) tuendelee kuahirikiana katika kutangaza vivutio mbalimbali vinavyopatikana hapa nchini,"alisema.

Mmoja wa waonyeshaji wa bidhaa wa sekta ya utalii kutoka kampuni ya Serengeti Balloon Safaris, Gloria Kanza, alisema maonyesho hayo yanatija kubwa katika kukuza sekta ya utalii na uchumi nchini, ambapo wamekutana na wanunuzi mbalimbali wa kimataifa ambao wameonyesha nia ya kuleta watalii nchini.

HABARI KITAIFA

# Elimu mikopo kausha damu yashika kasi

**Na Mwandishi Wetu,** KIGOMA

ELIMU kuhusu mikopo ya fedha kutoka katika taasisi zilizosajiliwa na wananchi kujiepusha na mikopo kutoka taasisi zisizosajiliwa na hatimaye kusababisha maumivu kwa wananchi, maarufu kama kausha damu, imezidi kutolewa kwa wananchi.

Baada ya elimu hiyo kutolewa katika mikoa ya Kagera, Katavi na Geita, sasa imewafikia wananchi wa Kigoma.

Katika utoaji wa elimu hiyo, wananchi wa wilaya ya Kakonko, mkoani Kigoma, wamepewa ujuzi na maarifa kuhusu mikopo hiyo huku wakitakiwa kuacha tabia ya kukopa fedha kwenye taasisi zisizo na leseni za kutoa huduma za fedha ili kuepuka kuingia kwenye migogoro wakati wa kurejesha mikopo.

Rai hiyo ilitolewa juzi na Mkuu wa Wilaya ya Kakonko, Kanali Evance Mallasa, alipokutana na timu ya wataalamu ya Wizara ya Fedha ambayo inaendelea na utoaji wa elimu ya fedha kwa wananchi wa makundi mbalimbali katika mkoa wa Kigoma.

Kanali Mallasa alisema wananchi wengi wa Kakonko, wakiwamo watumishi wa umma, wanakabiliwa na changamoto ya kuomba mikopo umiza, maarufu kama kausha damu, kwenye taasisi zisizo rasmi jambo linalosababisha kutapeliwa na kuingia kwenye wimbi la umaskini.

"Mikopo hii ya kausha damu kwa kweli imekuwa ikiwaumiza sana wananchi na watumishi wa serikali kutokana na riba kubwa inayowekwa na wakopeshaji pasipo kufuata taratibu za mikopo jambo ambalo halina afya kwa ustawi wa wananchi wetu," alisema Kanali Mallasa.

Alisema mikopo inayotolewa mtu akifuatilia hawezi kuona mikataba ambayo hutolewa kwa uwazi bali imejificha na kusababisha wananchi kutoa marejesho makubwa kutokana na riba kubwa, hali ambayo inawaumiza.

Kanali Mallasa aliwashauri watumishi na wananchi wote kwa ujumla kukopa kwenye taasisi rasmi kwa sababu kuna taratibu zinawekwa na zinafahamika kwa wananchi kwa uwazi.

Ofisa Usimamizi wa Fedha katika Idara ya Uendelezaji wa Sekta ya Fedha Wizara ya Fedha, Stanley Kibakaya, aliwataka wananchi kuwa na utamaduni mzuri wa masuala ya kutafuta na kutumia fedha.

"Nidhamu ya fedha ni pamoja na kile unachopata katika utendaji wa kazi katika biashara na utumishi kuendana na matumizi. Watu wengi wamekuwa na matumizi mabaya ya fedha. Anapata Sh. 10,000 lakini matumizi yake ni 15,000," alisema Kibakaya.

Alisema madhara ya kutumia fedha zaidi ya kipato ni kuingia kwenye mikopo ambayo si salama, hivyo ni vyema wananchi kuwa na utaratibu wa kuandaa bajeti ili kile wanachopata kiwekewe utaratibu wa kutumia vizuri.

Mkazi wa kijiji cha Kabale wilayani Kakonko, Ernest Mboko, alisema elimu aliyopata imemfanya kuwa na uelewa wa kutafuta fedha, kuweka akiba na kufanya matumizi sahihi kulingana na mahitaji.

Timu ya wataalamu kutoka Wizara ya Fedha inaendelea na utoaji wa elimu ya fedha kwa wananchi katika mikoa mbalimbali ili kuhakikisha wananchi na jamii inapata uelewa na kujifunza namna bora ya matumizi sahihi ya fedha na kujiepusha na matumizi yasiyo rasmi.



Ofisa Usimamizi wa Fedha kutoka Idara ya Uendelezaji wa Sekta ya Fedha katika Wizara ya Fedha, Stanley Kibakaya, akitoa elimu kuhusu umuhimu wa mbinu na njia za kuweka akiba kwa wananchi wa Wilaya ya Kakonko, mkoani Kigoma, juzi. **PICHA: WF**

## Wapatiwa elimu usalama watalii

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

WANAFUNZI wa Taasisi ya Taaluma ya Wanyamapori Pasiansi mkoani Mwanza, wamefika katika kituo cha Polisi cha Utalii na Diplomasia jijini Arusha kwa ajili ya kujifunza namna kituo hicho kinafanya kazi ya kuwahudumia watalii na wageni wanaofika mkoani hapa.

Mkuu wa Kituo hicho, Mrakibu (SP) Waziri Tenga, alibainisha juzi kuwa wanafunzi hao wamepata fursa ya kujifunza mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na umuhimu wa kuzingatia usalama wa watalii na wageni pindi wanapowahudumia.

Aidha, SP Tenga aliwasihi wanafunzi hao kuhakikisha wanakwenda kutoa huduma bora kwa watalii kwa sababu wageni wengi huwa wanatarajia kuona wanapata huduma bora pindi wanapofika nchini.

Tenga aliwaeleza wanafunzi hao namna ambavyo kituo hicho kimeimarisha uhusiano mzuri kwa kushirikiana na taasisi zingine za sheria na za kimataifa lakini pia kampuni zote za utalii ili kufikia lengo la serikali kuhusu usalama kwa watalii wakati wote.

Mkufunzi kutoka chuo hicho, Grace Mahendeka, alsiema lengo la kuwaleta wanafunzi hao katika kituo hicho ni kupata uzoefu wa namna gani kesi mbalimbali za utalii zinashughulikiwa katika kituo hicho lakini pia kuimarisha mahusiano baina ya taaisisi hiyo na Jeshi la Polisi.

Naye Victor Christian, mwanafunzi toka katika chuo hicho, alisema wamejifunza mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja uhusiano mzuri baina ya polisi na kampuni za utalii na taaisisi zingine na kupata fursa ya kuona zinaendeshwa katika kituo hicho. Aidha, alibainisha kuwa elimu waliyoipata itawasaidia kuwa na uhusiano mzuri baina yao na taasisi mbalimbali likiwamo Jeshi la Polisi ili kuhakikisha watalii wanakuwa salama.

# Serikali kuanza mahojiano rasmi na wakimbizi

**Na Mwandishi Wetu,** KIGOMA

SERIKALI imetangaza kuanza mpango maalumu ifikapo mwakani kuhoji wakimbizi 158,902 walioko nchini katika kambi mbalimbali zikiwamo za Nduta, Nyarugusu na wanaohifadhiwa katika makazi ya Ulyankulu, Katumba na Mishamo pamoja na vijiji vya mkoa wa Kigoma.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhandisi Hamad Masauni, alisema hayo juzi baada ya kupokea taarifa ya Kikao cha Wataalamu wa Pande mbili baina ya serikali ya Tanzania na serikali ya Burundi, ikionyesha uwapo wa raia wa Burundi wanaogoma kurejea nchini kwao licha ya amani na utulivu kurejea kwao.

Kabla ya kikao hicho, serikali zote mbili zilitia saini taarifa ya pamoja ya makubaliano ya urejeaji wa wakimbizi ambapo upande wa Tanzania uliwakilishwa na Waziri Masauni Burundi ikiwakilishwa na Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Ndani, Maendeleo ya Jamii na Usalama wa Raia, Theofile Ndarufatiye.

Akizungumza katika mkutano na waandishi wa habari, Waziri Masauni aliweka wazi nia ya Tanzania kuendelea kusaidia nchi jirani zinapokuwa katika matatizo ikiwamo matatizo ya vita huku akitoa ahadi ya kuendelea kuzisaidia nchi hizo kupokea na kuhifadhi wakimbizi ambao wanakidhi vigezo vya kuwa wakimbizi. 'Tumefanya vikao mbalimbali na wenzetu kutoka serikali ya Burundi na wametuhakikishia uwapo wa amani na utulivu nchini Burundi. Lakini kuna baadhi ya wakimbizi wameonyesha nia ya kutotaka kurejea nyumbani na sisi kama serikali tutaendelea kuwaelimisha umuhimu wa kurejea nyumbani na kuungana na wenzao ili kuweza kulileteа maendeleo taifa lao.

"Kutokana na hali hiyo ya kusuasua kwa urejeaji wa wakimbizi hao, sisi kama serikali tumeona ni vyema mapema mwakani kuwahoji wakimbizi kutoka Burundi kwa nini wanasita kurejea nyumbani sambamba na kupima sababu watakazozitoa na kufanya uamuzi sahihi kwa nchi yetu," alisema.

Naye Ndarufatiye alisema serikali ya Burundi inawahakikishi wananchi wake kuwapo kwa amani huku akiishukuru Serikali ya Tanzania kwa wema na ukarimu wa kuwahifadhi raia wa nchi hiyo kipindi chote ambacho kulikuwepo na hali isiyoridhisha ya amani na usalama nchini humo.

Mkurugenzi wa Idara ya Wakimbizi kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Sudi Mwakibasi, alisema utaratibu huo wa kuwahoji utazingatia sheria na kanuni zinazosimamia masuala ya wakimbizi duniani.

Alisema kazi ya kuwahoji wakimbizi hao itaendeshwa kwa mkimbizi mmoja mmoja na atayethibtika ana haki ya kuendelea kupewa hifadhi ya ukimbizi, ataendelea kuwepo kambini. Alisema atakayethibitika kutokuwa na haki hiyo, atapoteza hadhi ya ukimbizi na atakabidhiwa barua ya kuondoka nchini.

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hatua ya kuzuia ukaguzi wa magari ya watalii ya kusifiwa

**SERIKALI** ya Awamu ya Sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan, tangu ilipoingia madarakani mwaka 2021, imekuwa ikihimiza maendeleo ya sekta ya utalii kwa kutangaza vivutio vilivyoko ili kuwavutia watalii wengi zaidi kuingia na kuchangia pato la taifa.

Katika kutimiza azma hiyo, Rais Samia alicheza filamu ya The Royal Tour ambayo imeonyesha vivutio mbalimbali kama vile mbuga za wanyama, magofu ya kale na fukwe zilizoko katika pwani ya Bahari ya Hindi na maziwa mbalimbali. Sambamba na filamu hiyo, serikali imefanya mageuzi makubwa katika sekta hiyo ambayo yamesababisha wageni kuongezeka na kutembelea mbuga za wanyama na maeneo ya kihistoria na pwani visiwani Zanzibar.

Kwa kuonyesha hilo, wakati akimwapisha Mkuu wa Mkoa wa sasa wa Arusha, Paul Makonda, Rais alimwagiza kiongozi huyo kuwa ana jukumu kubwa la kuendeleza sekta hiyo ikizingatiwa kuwa mkoa huo ni kitovu cha utalii.

Bila kusita, Makonda alianza kutekeleza agizo hilo, ikiwamo kuomba ushirikiano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kwa wawekezaji wa visiwa hivyo, kuipa Arusha kipaumbele katika ujenzi wa hoteli pia watalii kuanza Zanzibar na baadaye kutembelea mkoa huo au vinginevyo kadiri ya ratiba zao zitakavyokuwa.

Ombi hilo lilikubaliwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, kuwa ni wazo zuri na linalenga kuendeleza sekta hiyo na kuahidi kuwa serikali yake itazungumza na wawekezaji ili kupanua fursa za uwekezaji pamoja na kampuni za utalii visiwani humo kupanga mipango itakayowezesha watalii kufika Zanzibar na Arusha.

Pamoja na nia njema ya serikali katika kukuza sekta hiyo, kumekuwa na vikwazo mbalimbali ambavyo vinasababisha usumbufu kwa watalii na hata kuiweka nchi katika taswira hasi kimataifa, hivyo kuwafanya wasirudi tena au kuwakatisha tamaa wengine wenye nia ya kufanya hivyo.

Moja ya vikwazo hivyo ni ukaguzi wa mara kwa mara wa watalii wakiwa kwenye magari ama wanapotoka uwanja wa ndege au maeneo ya mipakani wakati wanapoingia kwenye miji ya utalii, hususani Zanzibar.


Kutokana na kuwapo kwa kikwazo hicho, Makonda ameagiza polisi kuacha kusimamisha magari ya watalii yanayoingia katika jiji la Arusha kuanzia Julai Mosi, mwaka huu na kusisitiza kuwa magari yanapoingia Arusha, yanakuwa tayari yameshakaguliwa katika mipaka na viwanja vya ndege, hivyo kukagua yakiwa ndani ya jiji ni kusababisha usumbufu kwa watalii.

Akizungumza jana katika maonyesho ya Karibu Kili Fair (KKF) yanayofanyika katika viwanja vya Magereza Kisongo, mkoani Arusha, yanayojumuisha zaidi ya kampuni 700 za kimataifa kutoka zaidi ya nchi 50, alisema watalii wanaingia nchini na kuingiza fedha, hivyo kuwakagua mara kwa mara ni kuwasababishia kero ambazo zina athari hasi kwa maendeleo ya sekta na taifa kwa jumla.

Hatua ya kuzuia ukaguzi wa watalii ndani ya jiji la Arusha ni ya kupongezwa kwa kuwa kilio hicho kimekuwa cha muda mrefu na kwamba katika baadhi ya maeneo kimekuwa kikiwafanya watalii waone adha hata wakati mwingine wamekuwa wakiombwa rushwa na baadhi ya askari polisi.

Ni dhahiri kwamba kuondolewa kwa kikwazo hicho kitawafanya watalii kuondokana na usumbufu waliokuwa wakiupata awali na sasa hatua hiyo itawezesha Tanzania kupata sifa njema itakayosaidia watalii zaidi kuingia nchini.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Vita dhidi ya mimba za wanafunzi iwe ya jamii nzima

Na Sabato Kasika

**WANAFUNZI** 194 wa shule za msingi na sekondari katika wilaya ya Momba mkoani Songwe, wamepata mimba ndani ya mwezi mmoja kitendo ambacho kinaonyesha kwamba vita dhidi ya tatizo hilo haijapatiwa ufumbuzi.

Taarifa ya mimba hizo ni kwa mujibu wa Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Daniel Chongolo, ambaye anakemea uwapo wa mimba za utotoni, hawa kwa wanafunzi na kuahidi kuchukua hatua za kisheria.

Wakati kukiwa na taarifa ya mimba za wanafunzi wilayani humo, hivi karibuni iliripotiwa na gazeti hili kuwa wanafunzi 196 wilayani Iramba mkoani Singida nao walipata mimba na wengine 69 kuolewa.

Matukio hayo ni kipindi cha miezi 12 ya mwaka jana, ndivyo Ofisa Ustawi wa Jamii wilayani humo Happiness Alex, alikaririwa akisema katika kikao cha Kamati ya Ulinzi wa Mwanamke na Mtoto.

Hayo ni maeneo machache tu ya nchi. Hivyo nikirejea katika hoja yangu, ni kwamba kumekuwapo na sababu mbalimbali zinazotajwa kuchangia mimba hizo, miongoni mwake ikiwa ni baadhi ya wazazi na walezi kushirikiana na 'wahalifu'.

Kama hilo lina ukweli ndani, ninadhani ni vyema sasa wabadilike, wawaache watoto watimize ndoto zao katika elimu badala kuwaingiza kwenye mambo ambayo si ya umri wao ikiwamo kuwaozesha.

Vilevile, ni vyema jamii nayo ikahusika katika vita hiyo ili kusaidia kuwabana wale wanaochangia kuwapo kwa mimba hizo, kwa kutoa taarifa kwenye vyombo vya dola ili wahusika wakamatwe.

Jamii ikihusika katika vita hiyo, itakuwa ni rahisi kuwabaini wazazi na walezi ambao hawaoni umuhimu wa elimu na ambao wanashirikiana na wahalifu ili nao washughulikiwe haraka iwezekanavyo.

Pamoja na kwamba kuna vishawishi vingi vinavyochangia uwapo wa mimba ikiwamo shule kuwa mbali, ukosefu wa mabweni, bado wazazi, walezi na jamii, wana sehemu ya kufanya ili kuwaepusha watoto wao.

Hatua hizo ziende sambamba na kukaa na watoto wao na kuelimisha kuhusu madhara ya mimba za utotoni na mambo mengine ya afya ya uzazi, si kulea matatizo ambayo mwisho wake ni kukatisha masomo. Kwa kuwa tizo la mimba kwa wanafunzi ni la jamii nzima, kila mmoja wetu kama mzazi au jamii ana wajibu kupambana na suala la mimba za utotoni kwa kila njia ili kumlinda mtoto wa kike.

Kumwingiza mwanafunzi kwenye masuala ya mimba ni kumpa mzigo ambao hana uwezo nao. Hivyo, wazazi, walezi na jamii kwa ujumla ni vyema kufuata maelekezo ya serikali ya kutatua mimba hizo.

Njia hiyo inaweza kukomesha mtindo wa baadhi ya wazazi na walezi wanaoshirikiana na wahalifu, kwani wakinyamaza, jamii inaweza kupaza sauti ili wahusika wakamatwe haraka iwezekanavyo.

Wote wakiwamo wazazi, walezi, jamii na viongozi, tuna wajibu wa kusimamia haki, hivyo ni vyema kushirikiana katika vita hii ya mimba za wanafunzi ili watoto wa kike waweze kutimiza ndoto zao katika elimu.

Novemba mwaka 2021, historia iliandikwa kutokana na uamuzi wa serikali kuruhusu kurejea shuleni kwa wanafunzi waliokatiza masomo kwa sababu mbalimbali ikiwamo mimba.

Uamuzi huo uliambatana na waraka uliotoa mwongozo wa wanafunzi hao walioacha masomo kurejea shuleni na kuendelea na masomo. Nilidhani uamuzi huo ungekuwa ni fursa kwa wanafunzi kutafakari na kuwa makini ili kuepuka mimba hizo.

Lakini ajabu ni kwamba tangu wakati huo, mimba shuleni zimeendelea kuwapo kana kwamba uamuzi wa serikali kuruhusu wale waliokatisha masomo kwa sababu ya mimba ni kama imeruhusu mimba ziendelee.

Wazazi na walezi wajitafakari katika jambo hili, wasaidiane na serikali katika vita ya mimba badala ya kuwa sehemu ya tatizo, kwa kukubali kupokea chochote kwa wale wanaowapa mabinti zao mimba

SAFU

FIKRA MBADALA

# Siri pekee ya mafanikio kimaisha ni hii



Pascal Mayalla

LENGO la vyombo vya habari ni kuihudumia jamii. Ukikutana na jambo fulani zuri, linaloweza kuisaidia jamii, unaliandika ili kushirikisha wengine. Leo nawaletea mada ngumu kidogo ya jambo linalohusu kupata mafanikio kwa kutumia kitu kinachoitwa 'manifestation'.

Kabla sijaendelea, naomba kutoa angalizo kwamba mada hii haina uhusiano na imani ya dini yoyote bali ni kwa ajili ya watu ambao 'open minded'. Hawa ni wale wanaofikiria wenyewe na kwa kina.

Mtu wa aina hiyo akiambiwa jambo lolote, kabla ya kuliamini, analifikiria kwanza kisha kulikubali na kuliamini.

Kinyume cha watu wa kundi hilo, wako watu ambao ni 'close minded', wale ambao wakiambiwa jambo, wanaamini moja moja na hawahitaji kufikiria.

Kwa mantiki hiyo, mada hii ni ya watu wanaofikiria lakini wale waliofikirishwa na kuziamini dini zao, hapa sii mahala pao.

Nasema hivyo ili tusije kuleta mabishano ya imani za dini. Soma andiko hili huku umeshikilia imani ya dini yako.

'Manifestation' ni kulidhamiria jambo kwa dhati ya moyo wako. Dhati hiyo ya dhamira yako na juhudi yako kulifanikisha, inazifungua nguvu zilizoko ndani yako na kulitimiza jambo lako na linakuwa.

Somo hili kama lilivyoandikwa na mwandishi Ingrid Clarke katika kitabu cha 'Seven Pillars of Manifestations', lina nguzo saba ambazo ni Msingi wa 'Manifestation', 'Sheria za Manifestation', Mitetemo ya 'Manifestation', Kuweka Nia, kuona kwa jicho la ndani, Kukuamini ni kweli, na mchakato wa utekelezaji wake.

Kwanza kabisa tujiulize 'manifestation' ni nini? Katika andiko langu kuhusu 'psychic powers', nilisema kitu chenye nguvu sana katika mwili wa mwanadamu ni nia (will power).

Wazungu wanasema "where there is a will, there is a way", msemo huu hata waswahili tunao, unaosema, "penye nia, pana njia".

Manifestation ni kitendo cha kutumia mawazo yako, kufungua milango ya nguvu zilizo ndani yako, kufanikisha mambo yako.

Dini zote zinatufundisha tumeumbwa na Mungu na kuelezwa huyo Mungu yuko juu mbinguni, peponi au ahera, hivyo ukifa bila dhambi utaingia mbinguni na kumwona Mungu.

Ukifa na dhambi, tunaamini kwamba utakwenda motoni kwa shetani kwenye jehanamu a moto wa milele. Kwa hiyo wengi wakisali wanatazama juu wakijua ni kweli Mungu yuko juu mbinguni kule mawinguni.

Ukweli ni kuwa mbinguni na motoni ni hapa hapa duniani. Kuna ulimwengu wa aina mbili, ulimwengu wa mwili na ulimwengu wa roho.

Mungu alimwumba binadamu kwa kufinyanga udongo, kisha akampulizia pumzi ya uhai, hivyo mwili wa binadamu una sehemu mbili, yaani mwili wa nyama na mwili wa roho.

Mtu anapokufa, japo wanaita amekata roho, kinachokufa ni mwili wa nyama tu ambao unazikwa na kurejea kuwa mavumbi lakini roho inatoka, na kurejea kwake.

Ndiyo mana kuna maneno yaliyozoeleka kwamba "sote ni wa Mungu na kwake tutarejea."

Hata ile siku ya mwisho ya ufufuko wa miili, miili inayofufuliwa ni ya roho. Hii mili ya nyama, mtu akifa ndiyo mwisho wake, hivyo wanaochoma, wako sahihi na wanaozika kwa heshima zote kwa masanduku ya gharama na kujengea makaburi, ni kujifurahisha tu nafsi zao. Mtu akiisha kufa, ile mwili hauna maana tena.

Sasa ile pumzi, roho ambayo Mungu amempulizia binadamu ni roho ya Mungu, hivyo kila binadamu anao uMungu ndani yake. Ile dhana kuwa Mungu yuko mbinguni ameketi kwenye kiti cha enzi, ni kweli lakini pia Mungu yuko ndani yako, kupitia roho yake, na hii ni ile kanuni ya uwapo wa Mungu ndani yako.

Kwa mantiki hiyo, 'manifestation' ni kitendo cha kumtumia Mungu aliyeko ndani yako, kumtuma akunyooshe mambo yako.

Kwa mantiki hiyo, binadamu tuna nguvu za kufanya mambo mengi, lakini wengi hawajijui kama wanazo.

Wale wahubiri wa miujiza ya uponyaji, wanatumia uwezo wao kukumanifestia. Kinachokufanya ni imani yako na nguvu zilizo ndani yako na si nguvu za muhubiri.

Kwa vile tumepewa nguvu hizi bure, kuzitumia pia ni bure. Unachotakiwa kufanya ni kuamini tu.

Baada ya kusoma kuhusu 'manifestation' nikaona ni jambo jema, nimeamua kuwashirikisha watu wazitumie nguvu zilizo ndani yao kufanya mambo makubwa na kujiletea maendeleo.

Mada hii ya 'manifestation', itakupa fursa ya kutumia nguvu ya mawazo yako kufungua nguvu zilizomo ndani yako kukuletea mafanikio kwenye maisha yako.

Kwa urahisi kabisa, kitu pekee unachotakiwa kuwa nacho ni imani, kuamini kuwa unaweza.

Umeumbwa na nguvu na uwezo wa Kimungu uliomo ndani yako na unaweza kuufungulia na kuutumia kujipatia mafanikio na kujiletea maendeleo.

Nguvu ya 'manifestion' ni kutumia tu mawazo, kutengeneza ndoto za mafanikio na kutumia nguvu iliyomo ndani yako kuifanya ndoto yako iwe kweli, hivyo kutimiza ndoto yako.

Mfano, unataka kupata fedha nyingi, uwe Tajiri. Kupitia 'manifestation', unawaza tu jinsi ya kupata pesa kisha unaamini utapata pesa. Unaweka juhudi kwenye kutafuta pesa, kisha nguvu za Mungu zilizomo ndani yako zitakufungulia milango yako ya kupata pesa, hatimaye utapata pesa na kuuaga umasikini.

Upataji pesa kupitia 'manifestation', si kuamini tu na kulala kitandani kisha ukiamka asubuhi, unakuta umeletewa pesa chini ya mto! Katika kupata mafanikio kupitia 'manifestation', kuna misingi yake saba ambayo ni sheria, kanuni zake na utaratibu wake wa utekelezaji, hivyo lazima ufanye bidii kukipata kile unachotaka.

Tukutane wiki ijayo, nitakapokuletea kwa undani misingi saba ya 'manifestation'. Kitu muhimu ni kukumbuka kuwa kila binadamu amekuja duniani akiwa mtu na ataondoka mtupu.

Kupata na kukosa, ni juhudi tu na maarifa kama haya.

**Wasalaam**
**Paskali**
**0754270403**

# Walimu wapewa mbinu kuhusu ufundishaji

**Na James Mwanamyoto,**
KALIUA

NAIBU Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia Elimu, Dk. Charles Msonde, amesisitiza walimu wa shule za msingi na sekondari nchini kuzingatia uwezo wa wanafunzi wanapofundisha.

Kwa kufanya hivyo, amesema kutawawezesha wanafunzi kupata elimu na ujuzi stahiki kama ilivyoainishwa kwenye mtaala mpya ulioanza kutekelezwa Januari, mwaka huu, kwa madarasa ya awali, msingi na sekondari.

Dk. Msonde alitoa wito huo kwa walimu akiwa katika Shule ya Sekondari Usinge, wakati wa kikao kazi na baadhi ya maofisa elimu kata, wakuu wa shule, walimu wakuu na walimu katika Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua mkoani Tabora.

"Mwalimu unapofundisha watoto darasa lolote hata kama umeandaa mpango kazi, maazimio ya kazi na andalio la somo, unapaswa kukumbuka kuwa ufundishaji wako unategemea uwezo wa watoto unaowafundisha," alisema.

Dk. Msonde alisisitiza kuwa serikali inataka mabadiliko ya vitendo kwa walimu, hivyo walimu wanapaswa kuamua kuachana na mazoea ili wafundishe watoto kwa ufanisi na kwa kuzingatia weledi.

Alisema walimu hawana budi kuamini kwamba kuna changamoto katika ufundishaji wao kwa sababu haiwezekani mwalimu afundishe watoto Kiingereza mwaka mzima alafu wasijue kusoma, kuandika na kuzungumza, hivyo kusababisha kupata ufaulu usioridhisha katika matokeo ya mtihani wa kidato cha nne.

"Walimu tukiamini kwamba tuna changamoto, tuchukue hatua ya kubadilisha mitazamo yetu na kufanya tofauti na mazoea ambayo yametukwamisha na kutufikisha hapa tulipo," alisisitiza.

Ofisa Elimu wa Mkoa wa Tabora, Juma Kaponda, alisema anatamani walimu wa Kaliua na maeneo mengine nchini watekeleze hata robo ya maelekezo aliyoyatoa Dk. Msonde ambayo yamelenga kuleta mapinduzi katika sekta ya elimu kama ilivyokusudiwa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Dk. Msonde ameanza ziara ya kuhimiza uwajibikaji kwa walimu mkoani Tabora kwa kufanya vikao kazi viwili na maofisa elimu kata, wakuu wa shule, walimu wakuu na walimu katika Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua.

# Serikali yashauri watoto wafundwe uwekaji akiba kwa maisha ya kesho

**Na Mwandishi Wetu,**
SUMBAWANGA

SERIKALI kupitia Wizara ya Fedha imewashauri wazazi na walezi kuwafundisha watoto kuwa na utamaduni wa kujiwekea akiba ili kuwasaidia katika maisha yao ya baadaye.

Rai hiyo ilitolewa juzi na Ofisa Mkuu Mwandamizi Idara ya Uendeshaji wa Sekta ya Fedha katika Wizara ya Elimu, Salim Kimaro, wakati wa semina zinazoendelea katika miji na vijiji mkoani Rukwa.

Kimaro alisema kuwafundisha watoto kuweka akiba kutawajengea mfumo madhubuti wa kujenga uhakika wa masuala ya kifedha.

"Watoto wengi wamekiri kwamba walikuwa hawafahamu kwamba wanapopewa pesa wanatakiwa watumie kiasi na kiasi kingine waweke kama akiba ili siku wazazi wao wanapokosa pesa za kuwapa waweze kuzitumia," alisema

Kimaro alisema kwa sasa kuna taasisi mbalimbali kama vile benki zinatoa elimu kwa watoto kuhusu namna ya kuweka akiba, hivyo ni muhimu kwa wazazi na walezi kutumia fursa hizo kwa ajili ya watoto wao.

Akifunsisha katikaemina hiyo wilayani Sumbawanga, Kimaro aliwataka Watoto kuanzia ngazi ya shule kuwa na tabia au utamaduni wa kupanga bajeti na kwamba ili wapate akiba ya kuweka, inabidi fedha wanayopewa na wazazi au iliyopangwa kununua vitu, ipangiwe bajeti kwanza kwa vitu vilivyopangwa kununuliwa na itakayobaki iwekwe akiba.

Pia alisema kuweka akiba ni njia za kuondokana na madeni yanayotokana na matumizi ya kila siku pamoja na gharama nyingine za maisha.

# Ujenzi wa zahanati ukombozi wananchi

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

MRATIBU wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) Tunduru mkoani Ruvuma, Muhidini Shaibu, amesema ujenzi wa zahanati katika kijiji cha Mkapunda, unaotekelezwa na mfuko huo ni ukombozi kwa wananchi kwa kuwa awali eneo hilo halikuwa na huduma hiyo.

Shaibu alisema hayo jana ofisini kwake na kubainisha kuwa kwa sasa mradi huo uko katika hatua za mwisho ili kukabidhiwa serikalini kwa ajili ya kupeleka wataalamu wa kutoa huduma.

Alisema katika utekelezaji wa mradi wa kunusuru kaya maskini, serikali ilipeleka mradi wa ujenzi wa zahanati hiyo wenye thamani ya Sh. 92,410,714.29 baada ya kubaini kuwapo uhitaji mkubwa katika kijiji hicho.

Wakizungumzia mradi huo kwa niaba ya wananchi, Alifa Achieya na Mtendaji wa Kijiji, Evodia Nchimbi, walipongeza TASAF kwa kuwajengea zahanati zikiwa ni juhudi za serikali kusogeza huduma kwa wananchi na kuwapunguzia adha ya kusafiri umbali mrefu kutafuta huduma ya afya.

Nao Salima Abdalah na Hamis Leonard, walisema kabla ya ujenzi huo, walikuwa wanapata wakati mgumu hasa ilipotokea watoto wanaugua, kwa kuwa walitakiwa kuwasafirisha umbali mrefu kwenda katika zahanati ziliko zaidi ya kilometa sita.

Katibu wa usimamizi wa mradi huo, Asina Joseph, alisema pamoja na mambo mengine, aliwapongeza wananchi wa kijiji hicho kwa ushirikiano waliouonyesha wakati wote wa ujenzi bila kujali kuwa wakati mwingine walikuwa wanafanya kazi bila kula.

Alisema kilichobakia kwa sasa ni wananchi wa eneo hilo kuhamasishana kutumia zahanati hiyo ili kupata huduma ambayo ni ukombozi kwa jamii katika eneo lao.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji, Rajab Yasini, alisema kwa sasa mradi huo ambao serikali kupitia TASAF ilitoa zaidi ya Sh. millioni 92.410, umefikia asilimia 95.

Alisema kilichobakia hivi sasa ni hatua za mwisho za kupiga lipu na kupaka rangi ili wananchi waanze kupata huduma.

# ACT yalia maisha magumu vijana mtaani

**Na Halfani Chusi**

KIONGOZI Mkuu wa Chama Cha ACT Wazalendo, Dorothy Semu, amesema maisha baada ya vijana kuhitimu chuo ni msoto mpya mtaani usio na matumaini kutokana na ukosefu wa ajira.

Semu aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam katika mahafali ya wahitimu wa vyuo vikuu, ambao ni wanachama wa ACT Wazalendo, yaliyofanyika makao makuu ya chama hicho Magomeni.

Wahitimu waliohudhuria mahafali ni wakutoka vyuo vikuu mbalimbali nchini wakiwamo wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

Semu alisema Serikali ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), imeshindwa kutatua na kuleta majawabu ya kero zinazowakabili vijana nchini akisistiza la ukosefu wa ajira ni mojawapo.

Utafiti uliofanyika mwaka 2021 unatueleza kuwa katika Watanzania milioni 25.9 walio kwenye nguvu kazi ya taifa, ni milioni 2.3 tu sawa na asilimia tisa ambao wameajiriwa katika ajira rasmi na asilimia 91 ya wenye uwezo wa kufanya kazi hawamo kwenye mfumo rasmi.

"Kila mwaka wanaoingia katika soko la ajira ni Watanzania milioni moja na kati ya hao, wanaopata ajira ni 100,000 pekee na wengine 900,000 wanasalia mtaani bila ajira," alisema Semu huku akisema hali hiyo inatokana na sera za CCM.

Alisema hali ya vijana kukosa ajira mchini inatokana na serikali ya CCM kushindwa kujenga uchumi wenye kuzalisha ajira, kushindwa kuwekeza kwenye sekta zenye mnyororo wa ajira kama kilimo na viwanda.

Alisema kutokana na hali hiyo, iwapo chama hicho kitaingia madarakani, kitahakikisha kinalipia mafunzo kwa vitendo kwa fani zote kwa kipindi kisichopungua miezi sita ili wahitimu wote wapitie mafunzo kwa vitendo kikamilifu na kuweka utaratibu wa kutumia matokeo ya mafunzo kwa vitendo katika utoaji ajira.

Pia alisema chama kitajenga uchumi imara jumuishi ambao serikali ya sasa imeshindwa na inasimamia uchumi dumavu unaosuasua katika ukuaji wake na hivyo kuendelea kuwafukarisha watu na vijana kukosa ajira.

"Mbali na ajira, alisema ACT Wazalendo pia itafuta mikopo ya elimu ya juu ya miaka ya nyuma iliyotolewa kwa wanafunzi kwa ajili ya kulipia ada ya masomo na fedha za vitabu pamoja na gharama za mafunzo kwa vitendo kwa kila mwanafumzi anayedahiliwa kwenye chuo kikuu.

"Tutafuta mikopo yote ya wahitimu wote watakaoingia mikataba maalumu na serikali ya kufanya kazi kwa miaka mitatu mfululizo katika maeneo ya pembezoni na yenye mazingira magumu ya kazi," alisema.

Aliwataka Watanzania kujitokeza kukiunga mkono chama hicho wakati wa uchaguzi ili kitimize malengo hayo.



Mchuuzi wa ndizi mbivu akifanya biashara yake pembeni ya daraja katika eneo la Kimara Mwisho, Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam juzi, kitendo kinachoweza kuhatarisha usalama wake. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wadau wapendekeza hatua uvuvi endelevu Afrika

**Na Maulid Mmbaga**

WADAU wa uvuvi Afrika wamependekeza hatua mbalimbali zinazopaswa kuchukuliwa kwa ajili ya kuufanya uvuvi mdogo kuwa endelevu.

Miongoni mwa mapendekezo hayo ni kulinda maeneo yote ya uvuvi mdogo, kusaidia wanawake katika kazi wanazofanya na kujenga jamii ya wavuvi inayoweza kusimama vizuri na kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

Akiwasilisha mada juzi Dar es Salaam wakati wa mwendelezo wa mkutano wa uvuvi mdogo Afrika, Mwakilishi kutoka taasisi ya AFRIFISHNET, Patricia Maisha, alisema hatua hizo zinapaswa kuchukuliwa kwa haraka zaidi ili kufanya uvuvi kusaidia katika uchumi na kubadili maisha ya wananchi.

Maisha alisema kuna maendeleo yaliyofanyika lakini bado hayajajitosheleza na kwamba kuna kazi kubwa wanapaswa kuifanya, akieleza kuwa sio kazi ya Tanzania pekee bali ni Afrika nzima ili kufikia malengo ya Afrika katika sekta hiyo.

"Mimi naona kuna mkanganyika kwa sababu hatuwezi kuwa na mali alafu mataifa mengine watuelekeze namna ya kula/kutumia, wanatuaminisha kwamba samaki tunatakiwa kusafirisha, lakini la msingi tunapaswa kuona umuhimu wa kula samaki wenyewe Afrika," alisema.

Maisha aliongeza kuwa watu wanaoishi pembezoni mwa maziwa wanapaswa kujumuishwa katika sughuli zote zinazohusu uvuvi na kwamba wanapaswa kulindwa kwa sababu kuna athari zinatokea kama uchimbaji wa madini na mafuta, hivyo kusababisha athari za moja kwa moja katika sekta hiyo.

Aidha, alisisitiza kuwa usimamizi wa uvuvi unapaswa pia kuangaliwa ili kusaidia hali ya wananchi wanaoishi kukabiliana na uchumi, sambamba na serikali serikali kujenga taasisi zitakazosaidia uvuvi.

"Serikali na wadau wajenge jamii zitakazosaidia kutekeleza uvuvi endelevu, na kufanya tathimini ya utekelezaji wa kuhakikisha uvuvi mdogo unahusika katika kumaliza umasikini," alisisitiza.

Ofisa Uvuvi Mkuu kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Lilian Ibengwe, alisema asilinia 98 ya bidhaa za uvuvi zinatokana na wavuvi wadogo n kwamba katika kuwaendeleza, walianzisha utaratibu wa kuwa na vikoba ambavyo vitawasaidia kuwekeza na kupata fedha zitakazo wasaidia katika shughuli zao.

Pia alisema serikali imefanikiwa kupata njia ya namna ya kupata mikopo, vitendea kazi ikiwemo boti katika ziwa Viktoria, na katika kuhakikisha mchakato huo unakuwa endelevu wanashirikiana na wadau wakiwemo taasisi za ndani na mashirika ya kimataifa.

"Tunachotakiwa ni kuona namna ya kutekeleza njia sahihi za ushiriki kwa wadau wengine, na tunazishauri nchi za Afrika kuona namna tunaweza kuwa na sauti moja katika kuwasaidia wavuvi wadogo," alisema Lilian.

Aidha, alishauri jumuiya za Afrika kuwa na kikosi kazi kwa ngazi ya taifa kitakacho kuwa na maofisa kutoka serikalini, mashirika ya umma na binafsi na wavuvi, na kuwa na utashi wa kisiasa katika kushughulikia masuala ya uvuvi.

Pia alishauri kuwa na usaidizi wa kifedha katika utekelezaji wa sera za uvuvi na kufanya tathimini ya usimamizi wa utekelezaji kwamba unafanyika vizuri ama laa, na kwamba nafasi ya mwenyekiti katika jukwa ala utekelezaji mikakati ya uvuvi kuangalia mtu mwenye ushawishi.

MAISHA
JUNI 9, 2024
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili





## MAISHA NI NYUMBA


Usikurupuke kuuza nyumba




Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA





| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| C | | S | H | I | M | O |
| H | | | | T | | N |
| I | | J | I | I | | G |
| M | E | I | | K | O | O |
| B | | M | I | A | | Z |
| W | | B | | | | W |
| A | P | O | N | E | | A |


## FUMBO TOTO




Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

LAO, CHA, KOO, NOA, PENDO, AGANA, PANGA, NYOKA, CHOCHEA, ONDOSHA

## TOA TOFAUTI 5





## PAKA RANGI




## AMSHA AKILI

CHORA KWA KUUNGANISHA NAMBA KUANZIA 1-29 ILI KUPATA MCHORO KAMILI




TOFAUTI ya wazazi wa hapa nchini mtoto wa Tanzania na sehemu zingine wakati anapolala inakuwa kama hivi.

Marekani mtoto anapokwenda kulala huagwa na wazazi wake “usiku mwema mwanangu”

Uingereza wazazi wanamuaga mtoto wao “Pata njozi njema mwanetu”

Hispania anapokwenda kulala wazazi humuambia “usiku mwema mpendwa wetu”

Tanzania mtoto anapotaka kulala wazazi utawasikia “Kesho uamke mapema, hatutaki kusikia umechelewa na hela ya mihogo utaikuta mezani”

**SWALI**

Makaa ya mawe yanapatikana wapi hapa Tanzania?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Chanzo cha matatizo ya ndoa nyingi

KARIBU tena msomaji wangu tuendeleze mada kuhusu mitikisiko katika ndoa nyingi hata kusababisha zingine kubomoka na kila mwanandoa kuanzisha maisha mengine.

Wiki iliyopita tulijadili kwa nini shetani anashambulia sana ndoa? Nilitaja maeneo mawili, moja likiwa ni ujinga kwa baadhi ya wanandoa kutokuwa na maarifa namna ya kuishi katika ndoa.

Nikataja kupuuzia kanuni na misingi ya ndoa. Ukitaka uwe na ndoa yenye mafanikio na upenyo ni lazima utendee kazi kanuni na maelekezo yote yanayohusu ndoa.

Kwa bahati mbaya sana, watu wengi walioko kwenye ndoa hupuuza na kutupilia mbali kanuni na maelekezo waliyopewa siku wanafunga ndoa. Unapopuuzia kuombea ndoa yako, unapoanza kuona mabadiliko kwa mumeo au mkeo unapuuzia, hiyo itakugharimu baadaye.

Unapoota ndoto mbaya kuhusu mumeo au mkeo na kupuuzia, unaweza kujikuta unaingia kwenye matatizo makubwa ya ndoa baadaye.

Leo msomaji wangu tuende zaidi kuangalia chanzo cha matatizo ya ndoa. Nitajitahidi kuchambua vyanzo mbalimbali kadiri itakavyowezekana ili kusaidia wanandoa wengi ambao wana maswali mengi kuhusu mitikisiko katika ndoa zao wasijue cha kufanya.

Ni vema ikaeleweka kwamba kila tatizo la ndoa lina chanzo. Moja ni zile ndoa zinazofanyika pasipo Mungu kuhusika. (wakati ulikuwa adui wa Mungu). Watu wengi ambao huanza maisha ya ndoa pasipo kumshirikisha Mungu hukumbana na matatizo makubwa ya ndoa.

Siku zote msingi mbaya wa nyumba husababisha jengo kuwa dhaifu. Uhusiano wowote uliofanya wakati ukiwa adui wa Mungu huwa unafeli.

Mwanaume yoyote aliyeokoka na kuchukua maamuzi ua kumuoa binti ambaye hajaokoka, hujisababishia matatizo yeye mwenyewe huko baadaye. Ipo hivyo pia kwa binti kuolewa na mtu asiyeamini upo uwezekano wa matatizo baadaye.

Ndiyo maana Mungu akasema katika moja ya maandiko yake kwamba, “Msifungiwe nira pamoja na wasioamini, kwa jinsi isivyo sawasawa; kwa maana pana urafiki gani kati ya haki na uasi?”

Chanzo kingine ni pale ndoa inapofungwa kwa sababu tu ya kupata mimba kwa bahati mbaya/kumpa binti mimba. Watu wengi leo wameoana siyo kwa sababu walipanga, bali kwa sababu walilazimishwa kutokana na kupeana mimba kwa bahati mbaya.

Ndoa za aina hiyo hazifanyiki kwa sababu ya upendo bali kwa sababu ya matokeo ya kile walichokifanya. Aina hii ya ndoa inaitwa “zimamoto”. Kama umewahi kuona watu wa zimamoto wanavyofanya kazi kwa haraka sana na hawana muda wa majadiliano.

Binti anapopata mimba tu, kila mtu huanza kutaharuki. Wazazi wa pande zote mbili hukaa kwa haraka na kukubaliana ndoa ifungwe kwa haraka sana ili wasipate aibu.

**Nikataja kupuuzia kanuni na misingi ya ndoa. Ukitaka uwe na ndoa yenye mafanikio na upenyo ni lazima utendee kazi kanuni na maelekezo yote yanayohusu ndoa.**

Aina hii ya ndoa hutokana na tamaa ya mwili na siyo upendo wa dhati. Kama ungekuwa ni wa kweli binti asingejikuta ameingia katika matatizo ya namna hiyo.

Chanzo kingine ni kujihusisha kimapenzi kabla ya ndoa. Imebaika kwamba mapenzi kabla ya ndoa husababisha matatizo makubwa sana ya ndoa leo na kufanya mtu ajijengee majeneza ya kuzimu. Kama ukijenga jeneza kwa ajili ya ndoa yako, lazima utazikwa huko!

Vijana wengi leo wameshindwa kutunza ujana wao. Mabinti wengi nao wanaaibisha wazazi wao. Wengi wanaingia vyuoni, lakini wanapohitimu wanakuwa ni makahaba waliofuzu!

Chanzo kingine kinatokana na ndoa zilizofungwa baada ya mtu kwenda kwa mganga wa kienyeji. Ni kawaida katika tamaduni za baadhi ya wazazi wa Kiafrika kutembelea waganga wa kienyeji ili wawabashirie hatma za watoto wao.

Na mara zote, watu wengine wanaoamini huenda kwa wazazi wao na kuwaambia kwamba Bwana amewaongoza kuoa watu wa aina fulani. Ndipo wazazi huchukua majina ya wachumba wao na kuyakimbiza kwa waganga ili wajue kama ni mke/mume sahihi wa watoto wao.

Kama wewe ni mchunguzi msomaji wangu, wazazi wengi wa ki-Afrika, wana tabia ya kuchukua majina ya watu wanaowazunguka watoto wao. Kama ndoa yako ilifanyika katika misingi hiyo, haitafika mbali. Shetani ni mjanja sana. Anatumia historia ya maisha yako kupambana na maisha ya ndoa.

Leo tuishie hapa tuendelee wiki ijayo, nikutajie vyanzo vingine zaidi vinavyotesa ndoa nyingi katika jamii yetu. Bila shaka umejifunza kitu hapo. Je, una maoni au kisa cha kimaisha? **Ujumbe mfupi 0715268581.**

## NAWAZA KWA SAUTI
Na Godfrey Mushi



# Tunasita nini kuutangaza msitu wa Rau kimataifa?

MAONYESHO ya kimataifa ya utalii nchini, maarufu kama KARIBU KILI Fair 2024, yanayoendelea jijini Arusha, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), hajaupeleka sokoni msitu wa Rau, ambao una vivutio mbalimbali vya utalii wa asili.

Katika maonyesho hayo yanayokutanisha kampuni 700 za kimataifa kutoka nchi 50, wenye mamlaka walipaswa kutumia fursa hiyo kuijulisha dunia aina nyingine za vivutio katika msitu huo.

Iko nahau ya kiswahili inasemab mawazo huishi hata ukiwa kaburini hasa kwa mtu unayefikiri zaidi kuacha alama duniani.

Nimeanza na kumbukumbu hiyo kwa sababu nimemkumbuka mtafiti na mwanasayansi wa wanyamapori, Dk. Jane Goodall (sasa marehemu), aliyeanzisha wazo la kuwa na Roots & Shoots kwa ajili ya kuifanya dunia kurejea edeni na kuwa mahali pazuri pa kuishi kwa viumbe wote.

Wakati wa uhai wake akiwa Tanzania, alipigania sana ustawi na uhifadhi wa mazingira, wanyamapori na viumbe wengine walioko kwenye hatari ya kutoweka katika mapori tengefu, mapori ya akiba na hifadhi za taifa.

Aliijua Tanzania, alijua umuhimu wa rasilimali hii muhimu na adhimu. Kama ndivyo kwa kwa nini hatumuenzi kwa kuhuisha matamanio yake katika mazingira na uhifadhi wa Msitu wa Rau; ambao haujatangazwa na watalii wanaoingia nchini wakaamua kwenda kuutembelea na kujifunza mengi?

Nani anajua kwamba Hifadhi ya Msitu wa Rau, maarufu msitu wa Njoro, ulioko chini ya Wakala wa Misitu Tanzania (TFS), kwamba ndio msitu wa kwanza kuwa ndani ya mji nchini Tanzania?

Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) bebeni jukumu lenu la kisheria la kuitangaza Hifadhi ya Msitu wa Rau. Kuna mahali kama taifa tunajisahau kutangaza vivutio vyetu na tunachukulia eti ni vidogo vidogo, kumbe vikitumiwa vizuri vinaweza kuongeza mapato ya sekta ya utalii nchini.

Urithi huu tunapaswa kuvirithisha vizazi vijavyo, licha ya kwamba msitu uko katikati ya Mji wa Moshi, mkoa wa Kilimanjaro. Una maajabu mengi na haujatangazwa kama vivutio vingine vilivyoko kaskazini mwa Tanzania.

Ni eneo la maajabu, lina kitu kinachoitwa Ndiwa ya Uru, yaani Bwawa la Mizimu. Kihistoria hapo ndiko wananchi wengi hasa kabila la Wachaga, hupendelea kwenda kufanya matambiko yao.

Wenyeji wa Kilimanjaro, kuanzia Uru, Old Moshi, Kibosho, Machame na Siha na sehemu nyingine za Kilimanjaro, huenda hapo kufanya matambiko ili kuondoa mikosi, kupata mali au utajiri na kupona magonjwa.

Wako wanyamapori wa aina mbalimbali, isipokuwa wale wanyama wakubwa watano, lakini katika hifadhii hii kivutio kikubwa ni chatu mkubwa ambaye mara nyingi huwa anatokeza nje ya hifadhi kuelekea yalipo makazi ya wananchi ila hana madhara.

Chatu huyo huwa anatokea zaidi upande wa vijiji vya Msasani na Kaloleni. Huyo chatu ni mkubwa zaidi kiumbo na inaelezwa ana utamaduni wa kuonekana kila ikifika saa 5:00 asubuhi na si muda mwingine. Huwa anatoka msituni kwenda nje ya hifadhi eneo la uraiani anaota jua na watu wakitokea wakimuona wakipiga kelele anarudi msituni na hadhuri wanaopiga kelele.

Vijiji vitano vinavyouzunguka msitu huo na vinalindwa na historia ni Msasani, Mji Mpya, Mandaka, Mabogini na Msaranga. Msitu huo unaundwa na Kata za Mabogini, Msaranga na Mji Mpya.

Achilia mbali vivutio hivyo, hifadhi hiyo hiyo ya Rau, ina mti mkubwa ambao ni mti wa mvule. Ni mkubwa na wa kwanza kwa unene katika nchini zote saba za Afrika Mashariki. Huo mti haukuoteshwa ila ni mti wa asili, na una zaidi ya miaka 200.

Ukubwa wake ni kipenyo 300 na kama ukitaka kuushika ni lazima muuzunguke kwa kushikana mikono watu 13. Lakini hapo hapo pia, kuna miti ambayo haipatikani Afrika Mashariki yote, inaitwa Ostig Mamsoo. Zamani hiyo miti ilikuwepo nchini Kenya, na iliteketezwa na majangili na sasa imebaki pekee katika msitu wa Rau.

Inaelezwa kwamba msitu wa Rau kwa sasa una hekta meta 584, zamani ulikuwa na hekta meta 2,000 lakini kutokana na makazi ya jamii kuongezeka ilifikia mahali walipokuwa wengi kukajitokeza ugomvi ukamegwamegwa na kubakia kiasi hicho.

Mbali na mambo hayo, una utajiri wa chemichemi nyingi ambazo zinafua maji yanayotoka ndani ya hifadhi kwenda kulisha mashamba zaidi ya hekta 8,800 za mashamba ya umwagiliaji yanayouzunguka.

• **Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com**

# HARUSI



Ni kumbukumbu isiyosahaulika kwa Msonge Msilanga ni ilipofanyika sherehe ya kuagwa na wazazi wake Julai 27, 2022 katika ukumbi wa Prime Rose, Mbezi Dar es Salaam. Msonge alifunga ndoa na Yusuf Kaoneka.

# MITINDO

Na Moshi Lusonzo

## Hata wanasoka Bongo wanatupia

LICHA ya kujizolea umaarufu kwa kucheza soka, lakini kuna baadhi wanajulikana kwa kuvaa vizuri zaidi wanapokuwa nje ya viwanja vya mpira.

Kutokana na suala la mavazi kuingia katika mchezo wa soka, ndio maana baadhi ya mataifa wanawatambua wachezaji wao wa taifa wanaovaa vizuri na kupendeza.

Katika miaka ya hivi karibuni wachezaji wa Tanzania nao wamejikuta wakipamba vyombo vya habari kwa mavazi yao mara wanapoingia kambini.

Kitendo hiki kimewafanya wabunifu wa mavazi kutumia fursa kwa kuwavalisha wachezaji wa Taifa Star ili kukuza biashara zao na hivyo kuwaongezea kipato kwa wachezaji.

Kama wewe ni shabiki wa mitindo, basi utakubaliana nami pale wachezaji wanapoitwa kambini na kushuhudia kila mmoja akiingia na aina ya kipekee ya mavazi.





UREMBO

Na Mary Geofrey



# WEKA MIDOMO SAFI

UKIONA midomo yako imekuwa na rangi nyeusi na hujui cha kufanya, basi ukiungana na safu hii utajua namna ya kuondoa tatizo hilo.

Kuna njia ya asili ya kuondoa weusi kwenye midomo ndio hii, unatakiwa kuwa na karoti, bitiruti, asali na mafuta ya mzaituni.

Osha karoti na bitiruti, katakata, weka kwenye blenda kisha saga.


Huo mchanganyiko weka kwenye bakuli kisha weka vijiko viwili vya olive oil na asali, alafu changanya vizuri.

Kabla ya kupaka mchanganyiko huo, hakikisha unafanyia kwanza scrub ya mdomo.

Baada ya hapo chukua pamba, dumbukiza katika mchanganyiko wako alafu kuwa kama unapaka kwenye midomo yako polepole, kama ni asubuhi kaa nayo kwa dakika 20 baada ya hapo nawa. Ikiwa unapaka usiku paka na ulale nayo.

Kama una mstari mweusi katika midomo yako ongeza ndimu katika huo mchanganyiko wako.

Mchanganyiko huu unaweza kuuhifadhi kwenye friji kwa siku 12 na ukatumia bila shida yoyote.



MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Achari ya mbilimbi

ACHARI ya pilipili iliyotengenezwa kwa kutumia mbilimbi ni kichangamshi kizuri kutokana na kuongeza ladha katika chakula.

Watu wa maeneo ya pwani hasa waswahili hupenda kula vyakula vyao kwa kuongezea pilipili.

**Vitu vinavyohitajika**


Mbilimbi kiasi unachotaka, pilipili nyekundu vipande vitano, nyanya 2, kitunguu maji kikubwa kimoja, kitunguu saumu tembe nne, mafuta ya kupikia nusu kikombe, manjano kijiko kimoja na chumvi vijiko vya chai viwili.

**Jinsi ya kuandaa**

Loweka mbilimbi katika maji moto kwa dakika 10 kisha zitoe kwa kutumia kisu. Zipasue uzitoe mbegu kisha weka pembeni.

Chukua pilipili, vitunguu na nyanya kisha usage pamoja hadi kuvurugika.

Bandika sufuria jikoni kisha tia mafuta ya kupikia, yakishapata moto mimina rojo ya nyanya na vitunguu ulivyosaga. Acha rojo litokote kwa dakika tano kisha ongeza mbilimbi zako kavu.



Acha iive kwa muda wa dakika tano kisha epua na uweke pembeni ukisubiri vipoe.

Ikishapoa weka katika chombo chenye mfuniko na unaweza kuanza kutumia.

Unaweza kula achari hiyo kwa wali, pilau, matoke na kadhalika.



MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya

# USIKURUPUKE KUUZA NYUMBA

BIASHARA ya nyumba na uwekezaji wa majengo ya kisasa inaendelea kushika kasi kila siku nchini na duniani kote.

Lengo kuu la makala hii ni kupeana maarifa kuhusu mambo muhimu ya kuzingatia kabla ya kuuza nyumba kwa kujitathmini na kufanya uamuzi sahihi.

Mtaalam wa masuala ya ujenzi, Christian Kamase, anasema miongoni mwa mambo ya kuzingatia kabla ya kufikia uamuzi wa kuuza nyumba ni lazima utathmini lengo au sababu kuu ya kufanya hivyo na siyo kukurupuka.

Anasema wakati tulio nao biashara ya nyumba na uwekezaji wa majengo vinafanyika kwa mbinu za kisasa ambazo ni matokeo chanya ya ukuaji wa sekta hiyo ya ujenzi inayotokana na mapinduzi ya teknolojia mbalimbali duniani kote.

"Watu binafsi, kampuni na taasisi nyingi zimejitokeza kwa wingi kutumia fursa zinazoendelea kujitokeza kila siku kwenye biashara ya nyumba na uwekezaji wa majengo hususani kwa kuendesha kisasa zaidi kwa kutoa huduma za makazi na biashara kwa wadau mbalimbali,"anasema Kamase.

"Lakini kuna baadhi ya watu wamejikuta wakiingia kwenye uuzaji wa majengo au nyumba zao kutokana na changamoto mbalimbali wanazokabiliana nazo kwenye maisha, na ndiyo maana ninashauri kwamba ni muhimu sana ukajitathmini kabla ya kuuza nyumba yako, je ni kwa lengo la kibiashara au kutokana na kushindwa kukabiliana na msukosuko wa changamoto za maisha zinazokukabili."

"Kwa mfano hii ni Januari ambayo inajulikana misukosuko yake ya kifedha, kwa hiyo mtu bila tutulia na kujitathmini unaweza kujikuta unafanya uamuzi wa majuto baadaye," anasema.

Jambo linguine, anasema endapo kuna unazima wa kuuza ni vyema kabla ya kufanya uamuzi huo, kutathmini bei na gharama ya mauzo ambayo unayapeleka sokoni ili kukusaidia kufahamu kiwango halisi na faida au mapato utakayopata kwa kutimiza malengo unayokusudia.

Mtaalamu huyo anashauri kwamba ni muhimu kuzingatia kwa kuhakikisha nyumba yako inakuwa na muonekano mzuri wa kushawishi wanunuzi, na kwamba kama rangi yake ilikuwa imechakaa ni vema kuipaka upya pamoja na kuzingatia kuwa inakuwa safi wakati wote.

Anasema mvuto wa nyumba nao utakusaidia kukuongoza pia katika namna ya kufanya tathmini ya bei na itasaidia inunuliwe kwa muda mfupi.

Pia anashauri kwamba kabla ya kufanya uamuzi wa mauzo, ni vema kutathmini hali ya soko la nyumba na si kukurupuka.





# Zijue samani zisizo za kawaida

Na Restuta James



DUNIA ya sayansi, teknolojia, ubunifu na uvumbuzi imeendelea kuleta mageuzi kwenye sekta ya majenzi na mapambo ya nyumba, ikiongeza vitu vipya kila siku.

Moja ya mambo yaliyoongezeka ni kusambaa kwa taarifa za kila kinachofanyika sehemu mbalimbali na hivyo kurahisisha upatikanaji wa maarifa kuhusu jambo lolote, ukiwa sehemu yoyote na hii ndiyo inayodhihirisha kwamba dunia ni kijiji.

Katika miaka ya karibuni, kwenye maduka mbalimbali mitandaoni, baadhi ya wabunifu wa samani wametengeneza zinazoitwa 'zisizo za kawaida' ambazo zimebuniwa kama picha za wanyama au ndege wakiwamo wa kutisha.

Kwenye mitandao zimeonyeshwa samani zilizobuniwa kama tembo, simba, chui, fisi, nguruwe, mbwa, farasi, paka, sokwe na nyoka; huku nyingine zikionekana kama bundi, tai, tausi na mbuni.

Ziko pia zinazotengenezwa kwa mwonekano wa vifaa kama gitaa, kinanda, gari ya kifahari au muundo wa kiatu kizuri.

Katika samani hizo, zipo meza za chakula, kahawa, sehemu ya jiko na sofa za ndani na nje ya nyumba kwenye bustani au kibarazani.

"Kinachofanya ziitwe zisizo za kawaida ni kwa sababu baadhi zinatisha sana, kwa mfano utakuta kiti kimetengenezwa kama chatu aliyejiviringisha na sehemu ya kujiegamiza ni mdomo wake. Kingine unakuta ni bundi au simba anayenguruma," anafafanua fundi seremala Aloyce Michael.

Anasema ni watu wachache wanaopendelea samani za kutisha na kwamba badala yake wengi wanapendelea zaidi za wanyama wapole kama tembo kutokana na tabia za wanyama wengine kama mbwa.

# HABARI PICHANI



Ofisa Mkuu Mwandamizi Idara ya Uendeshaji wa Sekta ya Fedha kutoka Wizara ya Fedha, Salim Kimaro akitoa elimu ya fedha kuhusu akiba na bajeti kwa baadhi ya wanafunzi wa Shule ya Msingi Kipeta, wilayani Sumbawanga Vijijini, mkoani Rukwa juzi. **PICHA: WF**




Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango akihutubia wakati akifungua Kongamano la Kwanza la Kitaifa kuhusu Maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, katika Ukumbi wa Nkurumah, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam jana. **PICHA: OMR**



Naibu Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar, Dk. Mohamed Said Dimwa, akizungumza na Wasimamizi wa Uchaguzi na Mawakala wa Vyama mbali mbali vya Siasa vilivyoshiriki Uchaguzi mdogo wa Jimbo la Kwahani, Unguja jana. **PICHA: CCM ZNZ**



Mkurugenzi wa Shirika lisilo la kiserikali la Akili Platform Tanzania (APT), Roghat Robert (kushoto), akigawa majarida kwa watu waliotembelea banda la shirika hilo, katika maonyesho ya sita ya ufugaji ni mazingira yaliyoandaliwa na Chama cha Watunzaji wa Mazingira na ufugaji wa tija Tanzania (CHAMAUTA), jijini Dodoma hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Mchuuzi wa samaki (kulia), akiandaa kitoweo hicho kwa ajili ya mteja wake katika Soko la Buguruni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# HABARI KIMATAIFA



Baadhi ya nyumba zikiwa zimeteketezwa kwa moto na waasi wa ADF katika eneo la Beni mashariki mwa DRC. **PICHA: GETTY IMAGES**

## Waziri wa Ulinzi Israel kujiuzulu

**NEWYORK,** MAREKANI

WAZIRI wa Ulinzi wa Israel, Benny Gantz, anatarajiwa kutangaza kujiuzulu, wakati jeshi la nchi hiyo likiendelea kufanya mashambulizi mazito Ukanda wa Gaza, na kusababisha mauaji na majeraha.

Mwezi uliopita, Gantz alitangaza ataachia wadhifa huo ifikapo Juni 8, iwapo Waziri Mkuu Benjamin Netanyahu hatatoa utaratibu unaoeleweka ukilenga kumaliza vita vya Gaza.

Jana jeshi liliendeleza mashambulio kwenye eneo la al-Nuseirat , likisema linalenga miudombinu na ngome za Hamas.

Wizara ya Afya ya Ukanda wa Gaza ilisema kwa muda wa saa 24 zilizopita, Wapalestina 70 wakiwemo watoto wameuawa kutokana na mashambulio hayo, huku idadi ya vifo ikifikia zaidi ya 36,800.

Serikali ya Israel inakabiliwa na shinikizo kutokana na mwenendo wake katika operesheni ya kijeshi katika eneo hilo.

Kwa mujibu wa mashuhuda na ripoti za waandishi wa habari wa shirika la habari la AFP, mashambulizi ya Israel yalilenga maeneo tofauti ya Ukanda wa Gaza na kuelekezwa zaidi upande wa katikati mwa mji wa Gaza.

Mashambulizi hayo yanajiri, licha ya uchunguzi dhidi ya Israel baada ya ndege zake za kivita kufanya shambulizi kwenye shule inayosimamiwa na Shirika la Umoja wa Mataifa linalowahudumia wakimbizi wa Kipalestina UNRWA.

Wakati huo huo, Umoja wa Mataifa, umeliweka jeshi la Israel kwenye orodha ya wahalifu walioshindwa kuwalinda watoto mwaka jana.

Balozi wa Israel katika Umoja wa Mataifa Gilad Erdan, alisema aliarifiwa kuhusu uamuzi huo siku ya Ijumaa, na kuelezea uamuzi huo ni aibu.

Waziri wa Mambo ya Nje, Israel Katz alisema hatua hiyo itakuwa na madhara kwa uhusiano wa nchi yake na Umoja wa Mataifa.

Msemaji wa rais wa Palestina, aliliambia shirika la habari la Reuters kuwa uamuzi huo ni hatua ya hivi karibuni ya kuiwajibisha Israel kwa kile alichokiita vitendo vya jinai dhidi ya ardhi yao.

Maelfu ya watoto wameuawa na wengine wanahitaji msaada katika vita vinavyoendelea Ukanda wa Gaza dhidi ya jeshi la Israel na wanamgambo wa Hamas.

Orodha hiyo ya kila mwaka inayoandaliwa na katibu mkuu inahusu mauaji ya watoto katika migogoro na kunyimwa misaada ikiwamo shule na hospitali.

Israel itajumuishwa katika ripoti itakayowasilishwa katika Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa wiki ijayo.

Haijabainika mara moja ni ukiukaji gani ambao jeshi la Israel linashutumiwa kutekeleza.

Hamas na Palestina Islamic Jihad pia zitajumuishwa katika orodha hiyo, ilisema ripoti hiyo.

Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, alisema Umoja wa Mataifa umejiongeza kwenye historia mbaya na kwamba jeshi la nchi yake ndilo lenye maadili zaidi duniani.

Israel ilianza mashambulizi yake baada ya Hamas kushambulia watu karibu na mpaka wa Gaza Oktoba 7, mwaka jana na kuua watu 1,200 wakiwemo watoto 38 na kuwachukua mateka 252 .

Wizara ya Afya inayoendeshwa na Hamas Ukanda wa Gaza ilisema watu 36,731 wameuawa na Israel kutokana na mashambulizi ya mabomu ya ardhini.

Mwezi uliopita, Umoja wa Mataifa ulisema watoto 7,797 waliuawa wakati wa vita kulingana na data inayohusiana na miili iliyotambuliwa iliyotolewa na wizara ya afya inayoendeshwa na Hamas.

**BBC**

## Niger, Benin zaendelea kuvutana

**NIAMEY,** NIGER

MVUTANO wa kidiplomasia kati ya nchi za Niger na Benin umeongezeka baada ya kukamatwa raia watano wa Niger katika bandari ya Seme-Kpodji iliyoko nchini Benin.

Raia hao walikamatwa katika bandari hiyo baada ya kuingia kwenye eneo hilo bila kutaja utambulisho wao, kulingana na mwendesha mashtaka maalum katika Mahakama ya Makosa ya Kiuchumi na Ugaidi ya Benin, Elonm Mario Metonou.

Uhusiano kati ya nchi hizo mbili umekuwa wa wasiwasi tangu kufanyika kwa mapinduzi ya kijeshi nchini Niger ambayo yalimpindua Rais Mohamed Bazoum mwezi wa Julai mwaka jana.

Kumekuwepo na mgogoro kwa miezi kadhaa kutokana na tatizo la kufunguliwa kwa mpaka wao wa pamoja na upakiaji wa mafuta ya Niger yanayopitia bandari ya Benin na kupitia bomba la mafuta lililozinduliwa Novemba mwaka jana.

Serikali ya Niger bado inakataa kufungua mpaka wao na Benin, na Benin ikiweka masharti ya upakuaji wa mafuta ya kwenye bandari yake.

Kivuko pekee kilichoidhinishwa kati ya Benin na Niger ni mpaka unaounganishwa kwa daraja la Malanville, ambako upande wa Benin kuko wazi, lakini upande wa Niger ukiendelea kufungwa.

Jumatano jioni, televisheni ya taifa ya Benin ilitangaza kuondolewa kwa kizuizi kwenye mafuta ya Niger na kuthibitisha kwamba bomba la mafuta limefunguliwa tena.

Hata hivyo, tangazo hilo lilipendekeza nchi ya Benin kulegeza msimamo wake.

**RFI**

## Waasi waua watu 50 DRC

**KINSHASA,** DRC

ZAIDI ya watu 50 wameuawa katika mashambulizi yaliyofanywa na waasi wa ADF mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Waasi wa ADF wenye mafungamano na kundi la kigaidi la Dola la Kiislamu IS, waliwaua watu 13 katika shambulio la lililotokea Alhamisi katika vijiji vitatu katika Wilaya ya Beni katika jimbo la Kivu Kaskazini.

Kiongozi wa mashirika ya kiraia katika kitongoji cha Mamove,Kinos Katuo, alisema mauaji hayo yalifanyika nyakati za usiku baada ya waasi hao kuvamia vijiji.

Kundi la ADF kutoka Uganda, limekuwa tishio karibu miongo mitatu mashariki mwa DRC, licha ya majeshi ya nchi hiyo kwa kushirikiana na Uganda kuendesha operesheni za pamoja dhidi ya waasi hao.

**DW**

MAKALA

# KUNA MAJIRA YA KUPANDA NA KUVUNA



Na Magabilo Masambu

**Dunia hii imebaki na watu wachache sana wanaoweza kupanda mbegu kwa gharama ya muda na rasilimali zao. Ndiyo maana leo, hata ukimuuliza mtu kuhusu njia inayokwenda kwa Jakaya atakuuliza una shilingi ngapi? Maana yake mtu huyo hahitaji kupanda mbegu bali anataka kula mbegu papo hapo na kesho yake itajulikana akifika.**

KWENYE maisha ni muhimu kutambua kuwa kuna majira na nyakati tunazopitia. Majira hayo yanatutofautisha katika mambo mawili makubwa. Moja, wakati wa kupanda, pili wakati wa mavuno.

Kwa mantiki hiyo, usisahau kwamba kuna wakati ukiwa kwenye majira ya kupanda, mwenzako anaweza kuwa kwenye majira ya kuvuna. Hii ndiyo maana si kila wakati utaipima siku yako kwa mavuno.

Wakati mwingine, unatakiwa kuipima siku yako kwa mbegu nzuri ulizopanda na kama uko kwenye majira ya kupanda usichoke.

Fanya bidi zaidi ili wakati wako wa kuvuna ukifika, uwe na mavuno makubwa.

Katika vipindi hivyo viwili, kipindi kigumu zaidi ni cha kupanda mbegu. Kama tunavyofahamu, mbegu baada ya kupandwa ili iote lazima ioze kwanza, hivyo wakati wa kupanda ni kivumbi na jasho.

Hayo yote hayapaswi kuepukika ili baada ya muda mtu avune kwa furaha.

Wakati wa kupanda mbegu zenye kuleta manufaa makubwa ya siku zijazo, ndio wakati unaohitaji uvumilivu wa hali ya juu bila kuogopa kupoteza. Ndio wakati ambao mpandaji wa mbegu anaingia hasara ya kutosha na wakati mwingine kufikia kiasi cha kukata tamaa na pengine kuamua kutoendelea kupanda mbegu.

Kuna tatizo kubwa linalowakumba watu wengi hasa kipindi cha kupanda mbegu. Wengi wetu tunataka wakati tunapanda mbegu, tuwe tunakula sehemu ya mbegu zenyewe na wakati mwingine tunasema bila fedha hatuwezi kufanya kile na hili ndio wakati mashamba mengi hutupima kama tunastahili kupanda mbegu hizo katika mashamba hayo au la!

Dunia hii imebaki na watu wachache sana wanaoweza kupanda mbegu kwa gharama ya muda na rasilimali zao.

Ndiyo maana leo, hata ukimuuliza mtu kuhusu njia inayokwenda kwa Jakaya atakuuliza una shilingi ngapi? Maana yake mtu huyo hahitaji kupanda mbegu bali anataka kula mbegu papo hapo na kesho yake itajulikana akifika.

Leo ukimwambia mtu unafanya kazi mahali fulani au ulikuwa unamfanyia mtu kazi Fulani, swali la kwanza ni unalipwa shilingi ngapi? Anakulipa kiasi gani tunatazama sana tunapata nini leo wala hatuzami kuijenga leo ili kesho yetu iwe nzuri.

Siku hizi si fahari tena unapopata kazi fulani kuwajulisha ndugu na jamaa kwamba uko mahali fulani unafanya kazi, maana wazo la kwanza kabisa linalokuja vichwani mwao ni kwamba unalipwa pesa nyingi, hivyo wanaorodhesha matatizo yao ili uyatatue kwa sababu uwewaambia kuna mahali unafanya kazi.

Zamani kabla shetani hajahamia moja kwa moja kwenye pesa kuona ndiyo kila kitu, watu walifurahi na kukupongeza kwa dhati kusikia uko mahala fulani unahangaika leo ni tofauti, kwahiyo inawarazimu watu wengi kuficha shughuli wanazofanya.

Tumewahi kusikia mara kadhaa mtu anaulizwa fulani siku hizi yuko wapi na anafanya nini, utasikia tu jamaa yuko mjini na huwa hatujui anafanya nini.

Nachokusudia kusema ni kwamba, si kila anayefanya kazi mahala fulani anavuna wakati huohuo wengine wanapanda mbegu ili waje kuvuna baadaye, wewe pia panda mbegu sasa ili uvune siku zijazo na hapa mbegu inaweza kuwa mbegu ya wema au ubaya, ukipanda wema utavuma mema na ukipanda ubaya vilevile utavuna mabaya kwa wastani uleule, kumbe ni muhimu kupanda wema kwasababu waswahili husema wema hauozi.

Ukitaka kupanda mbegu sharti uandae shamba ufyeke nyasi na ulime, gharama za hapa na pale hazikwepeki, kuna wakati unahitaji kutumia chote ulicho nacho ili upande mbegu na kubaki hauna kitu, ipo siku hivyo unavyovipoteza vitarudi maradufu.

Ibrahimu alikuwa na mtoto mmoja tu, Mwenyezi Mungu akamwagiza enenda unitolee sadaka na kisha unifuate, japo sasa andiko hili pia limekuwa likitumiwa vibaya na baadhi ya watu wasiyo waaminifu katika imani ili kujinufaisha lakini hoja ya msingi inabaki palepale kwamba huwezi vuna mahala usipopanda.

Ushauri wangu. Moja tusihesabu kila tunachokifanya kwa maana ya kuleta manufaa wakati huohuo lazima tuwe na subra, katika kuyangoja mafanikio ya kesho.

Ukipanda leo ukavuna leo hakuna tatizo ni jambo jema, lakini usipovuna leoleo usikate tamaa na kuona wewe ni wa kupoteza tu Mungu yuko upande wako na yeye anayo majira yake hachelewi wala hawai.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**Dar es salaam-Tanzania**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Kisa cha mwanamume mkware aliyemtongoza mtalaka wake*



Na Adam Fungamwango

**Huyo huyo mkeo unayemdharau siku akikuponyoka ndiyo utaona thamani yake. Unaweza ukaja kumuona ni mrembo kuliko wale unaowakimbilia barabarani. Nitoe kisa kimoja cha mwanaume aliyekuwa na mke kwenye ndoa ambayo iligeuka kuwa ndoano.**

INAWEZEKANA kabisa waliosema hakuna mwanamke mbaya duniani walikuwa sahihi kabisa. Wanasema mwanamke kama anapewa matunzo, ikiwemo chakula, mavazi na akaishi kwa amani bila mikwaruzo, vituko na vipigo, basi anapendeza mithili ya malkia.

Kuna baadhi ya wanaume wanashindwa kutekeleza majukumu yao kwa wake zao na kuwafuata warembo wengine nje.

Lakini hakumbuki kuwa awali wakati anamtongoza na kumshawishi amuoe, alikuwa mzuri na mrembo, kuliko hata huyo msichana wa nje anayemfuatilia.

Sasa utajiuliza kwa nini anamuacha mkewe na kufuata wengine mitaani?

Kwanza ni tamaa, halafu pia amejisahau kumtunza mkewe kiasi kwamba amekuwa hapendezi tena kama zamani. Anawageukia wengine. Kilichotakiwa hapo ni kitu kidogo tu, kumjali na kumtunza mke ili arejee kwenye chati kama zamani. Baadhi ya wanaume wanaona kama wameshaanza kupitwa na wakati.

Waswahili wana msemo wao mmoja, kondoo haoni thamani ya mkia wake mpaka ukatwe.

Huyo huyo mkeo unayemdharau siku akikuponyoka ndiyo utaona thamani yake. Unaweza ukaja kumuona ni mrembo kuliko wale unaowakimbilia barabarani.

Nitoe kisa kimoja cha mwanaume aliyekuwa na mke kwenye ndoa ambayo iligeuka kuwa ndoano.

Mwanamke, alinyanyaswa, akapigwa, akadhalilishwa mpaka basi. Wakati mwingine alikuwa akifukuzwa usiku wa manane mvua ikimnyeshea. Mwanaume anamfukuza aende kwao. Anampiga na kumvutia nje, ambako kuna mvua, pia usiku mkubwa ambao una hatari ya kila aina. Kisha anafunga mlango. Mke atalala mlangoni hadi asubuhi, au atatafuta sehemu salama, asubuhi anarudi kule kule kwenye moto na mateso.

Hakuwa mjinga, alikuwa anatafuta muda na wakati sahihi. Akabeba kilicho chake akaondoka. Mume alidhani masihara, labda anaweza kurudi kesho au keshokutwa, wapi!

Hadi talaka ikatolewa.

Miaka mitatu baadaye jamaa alikutana na mwanamke mrembo njiani. Akapagawa, akamfuata na kueleza jinsi alivyojisikia faraja baada ya kumuona. Akamsifia alivyopendeza na akaomba awe mpenzi wake, ikiwezekana amuoe. Mwanamke akamuangalia, akatabasamu. Akaanza kufunguka moja baada ya lingine.

Majibu ya mwanadada huyo yapo katika wimbo wa Maquis Original, Sendema ya Moto, katika kibao chao kiitwacho, 'Kaiba', ambalo ndiyo jina ma mwanamke huyo. Wimbo huo ulitungwa na Tshimanga Kalala Asossa, miaka ya 1990.

"Unachoshangaa sasa ni nini we babu? Au unafikiri siyo mimi un'tamani tena eee, basi mimi ni yule yule Kaiba, uliyekuwa unanitelekeza, unanifukuza, kwa kashfa usiku mwingi mvua ikininyeshea bila huruma eee, mama mama.

Usinione hivi leo nimependeza, hii ni kazi nzuri ya mwezio babu kanithamini eee, basi mimi ni yule, Kaiba, uliyekuwa unamtelekeza, unanifukuza, kwa kashfa usiku mwingi mvua ikininyeshea bila huruma, mama.

Hata hivyo, mama ngoya ee, dunia kabla hujafa hujaumbika eee, namshukuru Mungu uliniacha salama eee, mama ngoya eee, ngoya, mimi kaiba nimetulia, mama ngoya eee, ngoya mimi Kaiba ee."

Haiitaji hata ufafanuzi kuwa kumbe mwanadada huyo ni yule aliyekuwa mkewe.

Mwanamke sasa akaanza kumfungukia yale yote aliyokuwa akimfanyia huko nyuma, mpaka mwanaume akaona aibu.

Aibu kubwa ilimpata kwa sababu kwanza alimtongoza mtalaka wake ambaye mwanzoni alimuona si lolote si chochote, lakini sasa amepata wa kumtunza amerudi kwenye chati, amekuwa mrembo kuliko mwanzo alipokuwa na umri mdogo. Pili kuonyesha kuwa alikuwa amemsahau kwa sababu ya urembo kuongezeka na kunawiri, kulimfanya aonekane ni kweli alikuwa hajui kutunza mke. Tatu maneno aliyopewa, mwenye hakuwa na hamu. Kila kitu kikaishia hapo.

Niwaambie tu wanaume kuwa hawawezi kushinda vita na mwanamke hata siku moja kama atakupania.

Wanaume wanane kwa kumi wamejikuta wakishindwa vita na wanawake kwa sababu ya mbinu zao kabambe ikiwemo kujifanya dhaifu, wao ni wepesi kudanganywa na kushawishiwa. Mtego huo.

Wanawake wengi wanajua wakati gani sahihi wa kumshinda mwanaume, ila wanaume wengi hawajui.

Mwanamke ni kiumbe anayetumia hisia zake kufricha hila, njama na akili zake usizitambue. Ni rahisi kulia au kuzuga katika mbinu ili uingie mkenge.

Ni kweli utamtesa, utamdharau na kumfanyia yote utakayoweza kumfanyia, ni mvumilivu wa mateso, lakini kumbuka ipo siku moja tu atakushinda kama anataka. Ukimtesa, akiamua kujibu mashambulizi wanajua muda sahihi wa kufanya hivyo.

Mara nyingi ni pale unapodondoka kinafasi, kicheo, kihadhi, uzee na kupoteza mamlaka na sauti mbele ya watoto wako mwenyewe.

Cha kufanya hapa kwa wanaume, ni kuwapenda, kuwajali na kuwatunza, na kwa sababu ni watu wa hisia, hupendezwa na hilo na kuwa wapole, wakarimu, huruma na upendo kwenye maisha yote ya ndoa.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

KIJANA Heri alikutana na msichana Nuru katika duka fulani maeneo ya Chanika, Dar es Salaam. Baada ya kuongea waliyoongea wakakubaliana kuonana siku ya Jumapili kwenye nyumba ambayo alimuelekeza aje kuulizia. Siku ilifika kama walivyoahidiana, masaa machache kabla ya kuwasili Heri alianza kusikia harufu mbaya chumbani kwake, ambayo kwa uzoefu wake aligundua ni ya panya aliyekufa. Akafanya kila kitu ambacho alidhani kinaweza kinaweza kumaliza tatizo kwani muda ulivyozidi kusonga mbele ndiyo harufu nayo ilizidi. Muda wa Nuru kufika ulikaribia. Njia mbadala aliyotumia kuondoa harufu ndiyo iliyoleta balaa zaidi.

# Harufu ya Panya-11

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

NITALIONDOA hilo tatizo, tena bure, sitaki hata pesa yako, huyu mwenzako ni rafiki yangu sana, huwa tunakutana njiani na tunaongea sana, ingawa nilikuwa sijawahi kufika kwake na yeye kwangu, leo hii alifika kwa sababu alinihitaji."

"Nashukuru sana mzee Rais kwa yote uliyoyafanya, nadhani sasa uende ukapumzike tu, mimi niache nimsindikize bibie huyu kituoni..." "Hapana kijana, hu inafaa amkodoshie bajaj, impeleke hadi kwao, siyo tena wa kwenda kuparamia mabasi, ashuke halafu aomgoze hadi nyumbani, au kupanda bodaboda kwa sababu anaweza kupata kizunguzungu. Ni wa kumkodishia bajaj." Akashauri mzee Raia. Ukaungwa mkono na Heri.

"Vipi uko vizuri?" Akauliza Heri wakati anampandisha bajaj. "Ndiyo ila kichwa tu ndiyo bado kinaniuma sana." "Pole, ngoja nikupeleke mpaka pale Chanika mwisho, nitashuka, nitakuacha ikupeleke nyumbani. "Ahsante sana." Kwa upande wa Nuru alianza kuona kama yupo sehemu sahihi. Kupata tatizo lile alilonalo hakufikiria kama angepewa huduma nzuri vile, kufarijiwa na watu ambao ni mara ya kwanza kwenda kwao, kukukutana na tatizo lile, kulitatua na kuahidi kulimaliza kabisa. Hakuona unyanyapaa wowote kwake. Walionekana kumsaidia kwa hali na mali. Mpaka anateremka aliendelea kuona upendo ule ule kwa Heri. Hiyo ilimtia moyo sana. Akajiambia moyoni kuwa atarejea tena ili aone mwisho wake. Safari hii atarejea akiwa na nia ya kwenda kuelezea sababu ya yeye kutupiwa jini alilonalo, na ikiwezekana mzee Raia amsaidie kwa jinsi atakavyoweza.

********************************

Kama alivyoahidi kurejea baada ya wiki moja alifanya hivyo. Alifika na kumkuta mwenyeji wake. Alifika nje. Akamwita Heri. Akatoka nje na kumkuta Nuru akiwa amesimama, akitabasamu. Akavuta picha siku ile ilivyokuwa, akatikisha kichwa, akataka kutabasamu, lakini akashindwa.

"Karibu ndani mgeni." Akakaribisha. "Ahsante, nimekaribia." Ilionekana kabisa Nuru hakutaka kuingia labda kutokana na kile kilichotokea wiki iliyopita.

"Pita ndani, leo sijawasha udi." Akasema huku akicheka na kumuambukiza Nuru. Akafanya hivyo kwa vitendo, akamshika mkono na kuongoza kuingia naye ndani.




**"Basi ule udi ndiyo ulionifanya nipandishe mwenzako!" Nuru alimpasha. "Hata mzee Raia aliniambia hivyo hivyo. Si unakumbuka siku ile kuna wakati tuliingia ndani wawili tukakuacha nje?" "Ndiyo."**

Baada ya mazungumzo ya zaidi ya robo saa hakuna kibaya kilichotokea, ndipo Nuru akauliza.

"Sasa kwa nini siku ile ulichoma udi chumbani?" Ilibidi Heri asimfiche kitu, akamuelezea sababu.

"Bibie, siku ile niliamka nikakutana na harufu ya panya, nikamtafuta wee wapi, na muda wa wewe kufika ukawa unakaribia. Nikaona ee, yaani siku ya kwanza tu mchumba akute harufu ya panya ndani kweli. Unajua nilitafuta kupita maelezo. Dakika za mwisho kabisa baada ya muda tuliahidiana na wewe kufika, nikaamua nikanunue udi dukani niuchome kwa ajili ya kuficha harufu kali ambayo ilikuwa kero kwangu, je mgeni ingekuwaje?"

"Basi ule udi ndiyo ulionifanya nipandishe mwenzako!" Nuru alimpasha. "Hata mzee Raia aliniambia hivyo hivyo. Si unakumbuka siku ile kuna wakati tuliingia ndani wawili tukakuacha nje?" "Ndiyo." Akajibu "Basi alikuja kuniambia kila kitu, sababu ya wewe kupandisha maruhani, na akanionya nisirudie tena kuwasha udi, au kupaka manukato siku nikiwa na wewe, au unayokuja hapa." Akamwambia na yeye mwenyewe akikumbusha alivyoonywa na mzee Raia siku ile.

"Kijana kama nilivyokwambia, yule jini alipanda kwa sababu ya ile harufu ya udi, kwa hiyo tahadhari kama utaendelea naye huyo msichana, siku anapokuja usiwashe kitu chochote kinachoitwa udi chumbani kwao, au manukato makali. Au wenyewe mwenyewe usipake pafyumu yenye harufu inayofanana na udi."

"Mhh! Pole sana!" Heri akaangua kicheko kupewa pole ambayo aliona hastahili "Pole nikupe wewe uliyekuwa umepandisha siku ile, siyo mimi." "Hakuna tabu uliopata siku ile, hadi nikarudi kwenye hali yangu ya kawaida." "We usiseme, ilibidi nimsake yule mzee, sijawahi kwenda kwake hata siku moja, tumezoeana tukikutana njiani tu, lakini hadi nilifika nyumbani kwake."

"Kwani nilikuwaje hadi ukaenda huko?" Akauliza Nuru huku akiwa amelala mapajani mwa Heri.

Walionekana kuzoeana sasa. Ndiyo maana kila mmoja akifunguka. "Kwani wewe ulijionaje? "Mimi mwenzako muda huo nakuwa sina hata fahamu. Likija hilo dubwana mimi sipo kabisa."

"Sasa usiombe ujione, utajiogopa mwenyewe." Alijibu na kusababisha Nuru aangue kicheko.

"Uliogopa eee?" Akauliza kwa utani. "Siyo niliogopa, nilikimbia kabisa." Kicheko kwa Nuru kikazidi kuongezeka. "We unafikiri mimi mpaka kutoka kwenda kumsaka mzee Raia mchezo? Yaani macho yalikutoka, ukawa unanitazama kama unataka kunirukia, nikanyanyata..." Heri alimuweka pembeni Nuru, akanyanyuka ghafla na kuanza kuigiza jinsi alivyofanya siku hiyo.

Aibu ya awali aliyokuwa nayo Nuru ilimuondoka kwa sababu alibaini kuwa Heri anampenda kweli, hivyo yale matatizo aliyoyapata ameyachukua kama yake pia, tofauti na alivyofikiria mwanzo kuwa angembwaga. Wakati akiingiza jinsi alivyokuwa akinyata, mpaka kuufikia mlango na kutoka nje mbio, Nuru hakuwa na mbavu kwa kicheko. Utani ulipoisha kila mmoja sasa alikuwa na hamu na mwenzake.

Mambo yaliyotokea wiki iliyopita yakawekwa pembeni. Kile kilichoshindwa kufanyika wiki iliyopita kikafanyika siku hiyo.

"Unajua pamoja na kukufuata wewe, lakini pia namhitaji mzee Raia kwa ajili ya jambo letu lile." Nuru alimkumbusha baada ya kutoka bafuni kujimwagia maji.

Wiki ikiyopita, alikwenda kuoga yeye kwanza, ili mwenzake aje baadaye, ila mambo yalivurugika alipomkuta ameshapandisha. Siku hiyo walikwenda kuoga wote.

Heri akakumbuka mazungumzo ya wiki iliyopita kati ya Nuru na mzee Raia.

"Mzee mimi ni msichana mdogo sana, wala sipendi haya madudu, yameniingia mimi mwenyewe nikiwa sijui. Na aliyesababisha haya yote ni mama wa kambo, hakuwa mtu mzuri kabisa..."

"Basi basi mama, leo usiongee sana maana bado hauko kwenye hali ya kawaida, unabidi ukapumzike nyumbani, ila baada ya wiki moja urudi hapa ili tulimalize hili tatizo."

"Yaani mzee kama unaweza kulimaliza mimi nitashukuru sana, maana rafiki zangu wameshawahi kunipeleka maeneo tofauti lakini imeshindikana. Mimi siitaki hali hii, nataka niwe mzima kabisa."

"Nitaliondoka hilo tatizo, tena bure, sitaki hata pesa yako, huyu mwenzako ni rafiki yangu sana, huwa tunakutana njiani na tunaongea sana, ingawa nilikuwa sijawahi kufika kwake na yeye kwangu, leo hii alifika kwa sababu alinihitaji." Akakumbuka.

"Ndiyo nakumbuka hilo. Sasa sijui twende wote kwake, au niende nikamwite!" "Mhh! Kwenda wote bado, ujue mimi nahitaji matibabu kutoka kwake. Hapa ndipo panafaa siyo kwake kila mtu ajue."

Wazo hilo likaungwa mkono na Heri. "Basi pumzika nikamwite."

ITAENDELEA JUMAPILI

# RIHANNA KWA NINI LAKINI?

MASHABIKI wa mwanamuziki maarufu visiwa vya Barbados, Rihanna, wamekuwa njia panda kufahamu kama nyota huyo ameacha muziki au la.

Tukio hilo limetokana na kitendo cha Rihanna kuvaa fulana yenye maandishi kifuani yaliyosomeka 'I AM RETIRED' akimaanisha yeye ni mstaafu.

Majuzi Rihanna na mpenzi wake, A$AP Rocky, na kuvalia fulana hiyo ambayo mashabiki wengi wanabashiri kwamba huenda msanii huyo amefika mwisho kisanaa.






# PREZZO AWATULIZA MASHABIKI

MWANAMUZIKI mkongwe kutoka Kenya, Jackson Ngechu Makini, maarufu kama Prezzo, amesema afya yake ni nzuri licha ya kuanguka jukwaani wakati akitumbuiza.

Prezzo alianguka ghafla na kuzirai wakati akiwatumbuiza watu waliohudhuria uzinduzi wa kipindi cha uhalisia cha familia ya msanii Bahati na Mkewe kitakachorushwa katika mtandao wa Netflix.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Prezzo amesema hana matatizo ya kiafya na kwamba tukio la kuanguka kutokana na uchovu baada ya kufanya kazi nyingi bila kupata mapumziko.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MINTEH KUTUA LIVERPOOL
NEWSACTLE inajipanga kumuuza winga wa Timu ya Taifa ya Gambia, Yankuba Minteh (19), baada ya nyota huyo kufanya vizuri katika usajili wake wa mkopo akiwa Feyenoord, kutokana na kumvutia kocha mpya wa Liverpool, Arne Slot. (**Telegraph - subscription required**), external

### WEST HAM YAMBANIA GARCIA
KLABU ya West Ham inajaribu kuzuia jaribio la Bayer Leverkusen kumsajili kiungo wa kati wa Girona na Timu ya Taifa ya Hispania, Aleix Garcia, mwenye umri wa miaka 26. (**Guardian).**

### SILVA AINGIA SOKONI
WEST Ham pia wanataka kumsajili winga wa Vitoria Guimaraes na Timu ya Taifa Ureno, Jota Silva, mwenye umri wa miaka 24. **(Teamtalk)**

### SPENCE ANOGEWA ITALIA
TOTTENHAM Hotspur inamwania, Djed Spence, mwenye umri wa miaka 23, anatarajia kujiunga na Genoa kwa mkataba wa kudumu baada ya beki huyo raia wa England kufanikiwa kusajiliwa kwa mkopo katika klabu hiyo ya Italia. (**Fabrizio Romano)**

### PARDEW AITAKA NEWCASTLE
KOCHA wa zamani wa Newcastle United na West Ham, Alan Pardew, mwenye umri wa miaka 62, anasema amevutiwa na kazi ya kuinoa Burnley.(**Talksport**)

### ADARABIOYO SAFI CHELSEA
MLINZI wa Fulham, Tosin Adarabioyo mwenye umri wa miaka 26, amefanyiwa uchunguzi wa kimatibabu kabla ya kuhamia Chelsea.(**Mail**)

### DYBALA KUTUA ENGLAND
MSHAMBULIAJI wa AS Roma mwenye umri wa miaka 30, Paulo Dybala, amesema kwa sasa yuko tayari kuhamia katika Ligi Kuu England msimu huu. (**Sky Sports**)

### LAMPARD ATAJWA BIRMINGHAM
KLABU ya Birmingham City imefanya mazungumzo na kocha wa zamani wa Chelsea na Everton, Frank Lampard. Lampard pia amezungumza na Burnley kuhusu nafasi hiyo baada ya kuondoka kwa Vincent Kompany aliyehamia Bayern Munich ya Ujerumani. (**Football Insider**)

### SOLSKJAER ATAJWA LEICESTER
KOCHA wa zamani wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, anajiandaa kurejea katika Ligi Kuu England kwa kujiunga na Leicester City kama kocha mpya. (**Sun**), external

### PALHINHA ANUKIA BAYERN
BAYERN Munich imerejea kufanya mazungumzo na Fulham kwa ajili ya kumnasa, Joao Palhinha, na iko tayari kutumia pauni milioni 38 ili kumpata kiungo huyo wa Timu ya Taifa ya Ureno mwenye umri wa miaka 28. (**Sky Sport Germany**), external

### TIERNEY KUREJEA CELTIC
BEKI wa kushoto wa Timu ya Taifa ya Scotland na Arsenal, Kieran Tierney, mwenye umri wa miaka 27, ameweka wazi yuko tayari kurejea katika klabu yake ya zamani ya Celtic na The Gunners wameridhia kupokea ofa kipindi cha majira ya joto. (**Football Insider**), external

### WHARTON ATAJWA CITY
MANCHESTER City imeweka wazi nia yake ya kumsajili kiungo wa England na Crystal Palace, Adam Wharton (20), kwa kumpa mkataba mrefu, lakini mchakato huo hautafanyika katika majira ya joto yajayo. (**Standard**), external

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI ULAYA




# MESSI : MADRID NDIO TIMU BORA DUNIANI

**MIAMI,** Marekani

● ● ● Lakini aeleza City inaonyesha kiwango cha juu cha...

LIONEL Messi amesema anaamini kocha wake wa zamani wa Barcelona, Pep Guardiola, ameigeuza Manchester City kuwa timu inayovutia zaidi kutazamwa, lakini amekubali Real Madrid ndio bora zaidi "kwa matokeo."

Guardiola aliiongoza City kutwaa taji la nne mfululizo la Ligi Kuu England mwaka mmoja baada ya kuiongoza timu yake kushinda mataji matatu ya kihistoria (Ligi Kuu England, Ligi ya Mabingwa Ulaya na Kombe la FA).

**Washindi wa LaLiga, Madrid waliishinda City katika robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya wakiwa njiani kunyakua Kombe lao la 15 la Ulaya mnamo Juni Mosi, mwaka huu.**

Alipoulizwa ni timu gani anaichukulia ni timu bora zaidi duniani, Messi aliiambia Infobae: "Ikiwa utazungumza kuhusu matokeo, ni Real (Madrid), ndio mabingwa wa sasa wa Ligi.

"Ukizungumzia suala la uchezaji, binafsi napenda timu ya Guardiola. Nafikiri timu yoyote aliyopo Guardiola itakuwa maalum kutokana na jinsi alivyo, anavyofanya mazoezi, anavyofanya kazi na anavyozifanya timu zake kucheza.

"Katika kiwango cha uchezaji kwangu, City ndio bora zaidi, na kwa matokeo ni Madrid."

Chini ya Guardiola, Messi alishinda mataji 14 akiwa Barca, yakiwamo mataji matatu ya LaLiga, mawili ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na makombe mawili ya Klabu Bingwa ya Dunia ya FIFA.

Messi kwa sasa anafanya mazoezi na timu ya Taifa ya Argentina mjini Miami.

Fowadi huyo wa Inter Miami atakuwa nahodha wa Albiceleste katika michuano ijayo ya Copa America itakayoandaliwa Marekani kuanzia Juni 20 hadi Julai 14, mwaka huu.

Washindi wa Kombe la Dunia la 2022 ndio wanaoshikilia Copa América kwa sasa.

"Nadhani Argentina inapendwa kila wakati," Messi alisema.

"Mashindano yanapoanza, iwe Kombe la Dunia, Copa América au chochote kile, Argentina ni mgombea kama Brazil na zaidi katika Copa America hii. Lakini nadhani leo timu za Amerika Kusini ziko imara sana.

"Uruguay ni nzuri sana, kama ilivyo kwa Colombia na Ecuador. Baadaye inakuwa vigumu sana kucheza michezo yote, lakini nadhani itakuwa Copa América iliyosawazishwa sana."

Messi mwenye umri wa miaka 36, alikiri kushinda Kombe la Dunia kumempa hali ya kuridhika lakini maisha yameenda kama kawaida.

"Ni wazi tumeshinda na kupata kila kitu katika ngazi ya kitaifa, ni uzoefu tofauti, kuna amani nyingine ya akili," alisema.

"Kuwa bingwa wa dunia nilijisikia kama nimeridhika. Nilifanikiwa kila kitu, niliweza kufikia malengo na ndoto niliyokuwa nayo.

"Ni kama kila kitu kilibadilika, lakini wakati huo huo hakuna kilichobadilika.

"Ndio, tulifanikisha lengo, na ni wazi ndicho tulichotaka zaidi, mimi, familia yangu na kila mtu."

# VARDY KUZEEKEA LEICESTER CITY




**LONDON,** England

MSHAMBULIAJI wa Leicester City, Jamie Vardy, ameongeza mkataba wa mwaka mmoja kusalia klabuni hapo hadi mwisho wa msimu wa 2024/25.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 37 ameiambia LCFC.com licha ya kufanya makubwa na kuisaidia klabu hiyo kurejea Ligi Kuu England bado anatamani kufanya zaidi huku akisisitiza umri si kigezo cha kumfanya asite kuendelea kusakata kabumbu.

"Niliyofanya msimu uliopita nimefurahishwa nayo ndio, lakini bado kuna mengi zaidi. Ninajitunza. Nimekuwa nikisema umri ni namba tu. Miguu yangu inajisikia vizuri ndiyo maana nitaendelea kucheza mpaka miguu yangu inaposema 'basi, game over'. Ipo siku itakuja, lakini sio sasa hivi."

Vardy aliweka wavuni mabao 20 katika michezo 37 akiwa na mchango mkubwa wa kurejesha mechi za Ligi Kuu England kwenye Uwanja wa King Power.

Mkataba huu mpya unamfanya mkongwe huyo kucheza msimu wake wa 13 klabuni hapo tangu alipojiunga na The foxes kutoka Fleetwood Town FC mwaka, 2012.



## England ipo tayari kwa Euro 2024

**LONDON,** England

GARETH Southgate amesema anaelewa mashabiki walivyoizomea England baada ya kupoteza mchezo wa kirafiki dhidi ya Iceland hapo juzi, lakini akaapa timu yake itakuwa tayari kwa michuano ya Euro 2024.

Simba Watatu hao walipoteza mchezo wao wa mwisho wa kujiandaa kwa kufungwa bao 1-0, Jon Dagur Thorsteinsson, akifunga bao dakika ya 12 ambalo lilitosha kuwapa wageni ushindi kwenye Uwanja wa Wembley.

Wengi wa umati wa watu 81,410 waliamua kuizomea England wakati wa mapumziko na muda wote wa mchezo ambapo Harry Kane na Phil Foden walipoteza nafasi nzuri lakini walifanikiwa kupiga shuti moja tu lililolenga goli, idadi chache zaidi katika mchezo tangu Juni 2021.

Alipoulizwa kuhusu hisia hasi za mashabiki, Southgate alisema: "Nimeelewa kabisa, hatukucheza vizuri vya kutosha kuwafanya wafurahi ndani ya mchezo.

"Tulikuwa na nafasi nzuri sana ambazo kwa kawaida zingemalizika ambazo zingeweza kutoa rangi tofauti katika mchezo na kuathiri hali ya kujiamini ya mpinzani. Lakini hiyo inaweza pia kuficha dosari ambazo zilionekana wazi usiku wa leo.

Kwa mtazamo wangu, nimejifunza mengi kutokana na mchezo huo lakini sijatishika na majibu ya mashabiki. Kuwa na mashabiki hapa ni wazi kunaleta mabadiliko makubwa lakini lazima uwape hatua ya kutosha ya goli, lazima ucheze vya kutosha."

England itamenyana na Serbia katika mechi ya ufunguzi ya Kundi C itakayochezwa Juni 16, mwaka huu.

## Hatima ya Ten Hag Utd bado

**MANCHESTER,** England

KUSUBIRI kwa Erik ten Hag kujua kama atasalia kama Kocha wa Manchester United kunatazamiwa kuendelea hadi wiki ya tatu zijazo, kwa mujibu wa ESPN.

Mabosi wa United, wakiongozwa na Mkurugenzi wa Michezo wa INEOS, Dave Brailsford, wanafanya ukaguzi wa mwisho wa msimu tangu ushindi dhidi ya Manchester City katika fainali ya Kombe la FA iliyochezwa mwezi uliopita.

Kulikuwa na uvumi uamuzi kuhusu mustakabali wa Ten Hag, kipengele muhimu cha ukaguzi ungewasilishwa wiki hii.

Lakini pamoja na mazungumzo bado yanaendelea, chanzo kiliiambia ESPN Ten Hag hajafahamishwa juu ya uamuzi wa mwisho.


Chanzo kimoja kiliiambia ESPN, United haijaweka muda wa mchakato huo na INEOS wanakataa kuharakishwa kufikia hitimisho.

Ten Hag amebakiza mwaka mmoja katika mkataba wake Old Trafford, lakini mustakabali wake uko shakani kufuatia msimu mbaya wa Ligi Kuu England.

Nafasi ya nane ya United ilikuwa nafasi yao ya chini zaidi tangu 1990 na walibeba Kombe la FA kwa sababu tu ya ushindi wa kushangaza wa mabao 2-1 dhidi ya City kwenye uwanja wa Wembley.

Lilikuwa ni taji la pili la Ten Hag kama kocha baada ya kunyanyua Kombe la Carabao Februari, mwaka jana.

Vyanzo viliiambia ESPN, United imetoa sauti ya mbadala zinazowezekana ikiwa ni pamoja na Thomas Tuchel, Mauricio Pochettino, Thomas Frank, Graham Potter, Kieran McKenna na Roberto De Zerbi.



HABARI MICHEZO

# SIMBA QUEENS YACHEKELEA UBINGWA, YAWAITA CHAMAZI

**Na Somoe Ng'itu**

WACHEZAJI wa Simba Queens wamesema wanasikia furaha kutimiza malengo yao ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania msimu huu na wanawaomba mashabiki na wanachama wao kujitokeza kusheherekea kombe hilo kesho kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Simba Queens imeivua ubingwa JKT Queens baada ya kuifunga Alliance Girls mabao 3-0 katika mechi ya ligi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza juzi na kufikisha pointi 46, ambazo hazitafikiwa na timu nyingine msimu huu.

JKT Queens ambayo jana iliwafunga Fountain Gate Princess mabao 4-0 yenye ina pointi37, kila timu ikibakiwa na michezo miwili ili kumaliza msimu wa 2023/2024.

Akizungumza baada ya mechi juzi, straika wa Simba Queens, Aisha Mnunka, alisema wanafuraha kufikia malengo yao na kama wasingetwaa ubingwa huo, wangeumia sana.

Mnunka amewaomba mashabiki wa Simba kujitokeza kwa wingi kesho katika mechi yao dhidi ya Fountain Gate Princess ili kuendeleza shangwe.

Alisema wametwaa ubingwa kwa sababu waliweka malengo hayo tangu kuanza kwa msimu huu.

"Tunafuraha sana kutwaa ubingwa, tumejisikia raha sana kufikia malengo, kama tusingeshinda leo (juzi), au tungeshindwa kutwaa ubingwa tungeumia sana kama tulivyoumia katika msimu uliopita, naombeni mashabiki mje kwa wingi Chamazi kama mlivyojitokeza hapa (Mwanza)," alisema straika huyo.

Naye golikipa wa Simba Queens, Caroline Rufo, alisema anafuraha kuisaidia timu yake kutwaa ubingwa wa ligi hiyo ambayo ilikuwa na ushindani.

"Nafurahia kutoruhusu bao katika mechi ya leo (juzi), na mechi nyingine kwa sababu zimesaidia timu yangu kupata ubingwa, tunawashukuru sana mashabiki wote kwa kutuunga mkono," alisema Rufo.

Kwa kutwaa ubingwa huo, Simba Queens itaiwakilisha Tanzania Bara katika mashindano ya Klabu Bingwa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA) ili kupata timu itakayochuana katika Fainali za Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake.




Wachezaji wa Simba Queens wakifurahia baada ya kuifunga Alliance Girls mabao 3-0 katika mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini, Mwanza juzi na kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania msimu huu. **PICHA: SIMBA SC**

# Nyota Simba wanukia Singida

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kutangazwa rasmi kutua katika kikosi cha Singida Black Stars, Kocha mpya, Patrick Aussems, raia wa Ubelgiji amesema anatarajia kusajili baadhi ya wachezaji ambao aliwahi kufanya nao kazi katika kikosi cha Simba.

Aussems ametumia Singida Black Stars akichukua nafasi ya Mecky Maxime.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Singida Black Stars, Kassano Jonathan, amesema kocha huyo anaendesha zoezi la usajili akishirikiana na menejimenti ili kupata wachezaji ambao watakifanya kikosi chao kuwa imara na tishio katika msimu ujao.

"Kwa sasa Kocha Aussems ndiye anayeongoza zoezi la usajili kwa kushirikiana na menejimenti, baada ya kumtangaza kuwa kocha mkuu. Tumeingia naye makubaliano ya mwaka mmoja ambao utaanza Julai Mosi, mwaka huu, na utamalizika Juni 30, mwakani," alisema Kassano.

Ofisa huyo alisema tayari Aussems ameshaanza mchakato wa usajili kwa kutuma mapendekezo ya wachezaji anaowataka wawe wamesajiliwa kabla ya yeye kuwasili nchini kuanza kazi.

Aussems amerejea nchini akitokea AFC Leopards inayoshiriki Ligi Kuu ya Kenya, ambayo imemaliza msimu huu ikiwa nafasi ya saba na pointi 36.

## Cadena aanika siri Simba kichapo 5-1

INATOKA UK. 24

tokea Azam FC.

Kufunguka kwa kocha huyo kumezidi kukoleza moto kwenye petroli, kwa sababu tayari 'joto limepanda' kufuatia Mwekezaji na Rais wa Heshima wa Simba, Mohamed Dewji 'Mo Dewji' kuwataka Wajumbe wa Bodi wa upande wake kujiuzulu ili kupisha mabadiliko, tayari baadhi wametii maombi hayo.

Taarifa zaidi kutoka kwa mwekezaji huyo zinasema ameamua kushiriki moja kwa moja katika kusuka kikosi imara uamuzi ambao anaamini utajenga timu yenye ushindani kama ilivyokuwa miaka ya nyuma.

Chanzo chetu kinasema Mo Dewji amewarejesha katika utendaji vigogo waliowahi kufanya vyema kuanzia zoezi la usajili akiwamo aliyekuwa Katibu Mkuu, Kassim Dewji, Swedi Mkwabi, Mulamu, Ngh'ambi na Crescentius Magori.

Simba ilikubali pia kichapo kutoka kwa watani zao katika mechi ya marudiano ya Ligi Kuu Tanzania Bara, ikitolewa mapema katika mashindano ya Kombe la FA lakini ikimaliza msimu huu katika nafasi ya tatu nyuma ya mabingwa, Yanga na Azam FC.

Kwa matokeo hayo, msimu ujao katika mashindano yanayoandaliwa na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika, Simba itawakilisha nchi kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika sambamba na Coastal Union ya jijini, Tanga.

Mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga na Azam FC, wao watachuana katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

## Yanga kutikisa nchi

INATOKA UK. 24

wote, ni wale viongozi ambao katiba inawatambua, ni viongozi watano kutoka katika kila tawi lililopo duniani kote ambapo Yanga inapatikana," alisema Kamwe.

Aliongeza mkutano huo utaongozwa na Rais, Hersi Said, na hii imekuwa ni utaratibu wa Yanga kukutana baada ya kumalizika kwa msimu.

"Ni nafasi nzuri ya kuwaambia wanachama namna msimu ulivyokuwa na yale ambayo walimwagiza (Rais), kuona utekelezaji wake, lakini ni sehemu ya kupanga mikakati kuelekea msimu mpya wa mashindano.

Katika mikutano yetu kila mwaka tunakuwa na 'sapraizi' sasa wanachama wanatakiwa kuja kwa wingi, na kufuatilia kuangalia safari hii tutawaletea nini," ofisa huyo alisema.

Naye Hersi alisema mkutano huo utakuwa na ajenda mbalimbali ikiwamo kuthibitisha hesabu za fedha zilizokaguliwa pamoja na kuwasilisha hesabu za mapato na matumizi ya klabu yao.

Hersi alisema wanaahidi wataendelea kuimarisha kikosi chao kwa kusajili wachezaji bora na wenye uzoefu watakaosaidia timu yao kufanya vizuri katika mashindano yote watakayoshiriki.

# Michezo

Jumapili Juni 9, 2024

Nipashe




Hatima ya Ten Hag bado UK. 22



Wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), wakifanya mazoezi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kabla ya kuwafuata wenyeji Zambia kwa ajili ya mechi ya Kundi E ya kusaka tiketi ya kufuzu Fainali za Kombe la Dunia itakayochezwa keshokutwa mjini Ndola. **PICHA: TFF**

# CADENA AANIKA SIRI SIMBA KICHAPO 5-1

**Na Adam Fungamwango**

## ● ● ● Kocha huyo asema kumpanga Manula ilikuwa 'shinikizo', ashauri panga...

IKIWA zimepita siku chache msimu wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2023/2024 kumalizika, Kocha wa Makipa wa Simba, Daniel Cadena, amefichua sababu iliyopelekea timu hiyo kupokea kichapo cha aibu cha mabao 5-1 kutoka kwa watani zao, Yanga ilitokana na shinikizo la kupangwa langoni, Aishi Manula.

Manula aliyekuwa majeruhi alisimama langoni Novemba 5, mwaka jana kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa na kufungwa idadi hiyo ya mabao.

Akizungumza na gazeti hili jana, Cadena, ambaye hana uhakika wa kuendelea na kibarua chake alisema shinikizo kutoka kwa baadhi ya viongozi lililazimisha Manula kupangwa wakati yeye alipendekeza kipa mwingine.

Cadena alisema ili Simba irejee katika ushindani, mabosi wanatakiwa kufanya mabadiliko 'makubwa' katika kila idara hasa kwa kuwaondoa watu ambao wamedumu kwa muda mrefu klabuni hapo.



Kocha huyo alisema 'watu' wakifanya kazi sehemu moja kwa muda mrefu huwa na tabia ya kuridhika.

Alisema kuelekea katika mchezo huo alikataa Manula asidake lakini ilitolewa amri kutoka 'juu' ikisema ni lazima kipa huyo adake na akaambiwa yupo tayari kwa mchezo, ingawa yeye (Cadena), alimfuata kipa huyo faragha na kumtaka asikubaliane na uamuzi huo.

"Najua uwezo wa makipa wangu, kabla ya mechi kocha mkuu huwa ananiuliza maoni yangu lakini kabla ya kucheza na Yanga hakuniuliza, alitoa amri tu, lakini pamoja na hayo nikamfuata Manula na kumwambia hatakiwi kucheza kutokana na hali ya kiafya, kilichotokea baada ya mechi matokeo yakawa tumefungwa 5-1," alisema kocha huyo.

Alishauri ili Simba ifanye katika msimu ujao, inatakiwa kutooneana 'aibu' na badala yake itafute watu wengine wenye weledi na uzoefu.

"Endapo kama watataka kufanikiwa inabidi wasafishe kila eneo kwa kuwaondoa watu ambao wamedumu ndani ya klabu kwa muda mrefu, unajua watu wakifanya kazi sehemu moja kwa muda mrefu huwa wanaridhika na hilo limeliona ndani ya klabu na kikosi," alisema kocha huyo aliyejiunga na Simba aki-

INAENDELEA UK 23

# Yanga SC kutikisa nchi leo

**Na Somoe Ng'itu**

MBALI na kutambulisha makombe iliyotwaa katika msimu uliomalizika, Yanga inajipanga kuwapa 'sapraizi' mashabiki wake katika mkutano mkuu wa wanachama utakaofanyika leo kwenye Ukumbi wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNICC) jijini, Dar es Salaam.

Yanga ikiwa chini ya Kocha Mkuu, Miguel Gamondi, imetetea taji la Ligi Kuu Tanzania Bara, Kombe la FA na kucheza hatua ya robo fainali ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema maandalizi kuelekea mkutano huo yamekamilika na kwa wakati mwingine muhimu wanatarajia kuelezea mikakati ya klabu kwa ajili ya msimu mpya wa mashindano.

Kamwe alisema mkutano huo unafanyika kwa mujibu ya katiba yao na amewaomba viongozi wa matawi wanaotambulika kuhudhuria bila kukosa.

"Tuko katika kumalizia maandalizi ya mkutano wetu utakaofanyika kesho (leo), hata hivyo hawaruhusiwi wanachama

INAENDELEA UK 23



GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >